# ATHARI ZA LUGHA YA KINYAMWEZI KATIKA KUJIFUNZA LUGHA YA KISWAHILI ENEO LA UTAFITI : URAMBO

**NYANDA JOSEPHINE**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA, IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2015**

**UTHIBITISHO**

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa ***Athari za Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya Kukamilisha masharti ya shahada ya MA. Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Dkt. Hanna Simpassa

**(Msimamizi)**

Tarehe

## HAKI MILIKI

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri kwa mfumo wowote ule au kutoa hata sehemu ndogo ya tasnifu hii kwa njia yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii na / au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

# TAMKO

Mimi **Josephine Nyanda** ninatamka na kuthibitisha kwamba Tasnifu hii iitwayo ***Athari za Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha Kiswahili*** ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa popote pale kwa lengo la kutunukiwa shahada yoyote katika Chuo Kikuu chochote.

Sahihi

Tarehe

# TABARUKU

Ninaitabaruku tasnifu hii kwa wanangu wapendwa

Tumaini

na

Mercy

Wana kila sababu ya kuhakikisha kuwa wanasoma kwa bidii na kufaulu vizuri sana!

## SHUKURANI

Ninapenda kumshukuru Mungu wangu kwa wema na ukuu wake kwangu.Ama kwa hakika yeye amejaa rehema , neema na uweza tele kwani amenijaalia uhai na ufahamu ulioniwezesha kukamilisha kazi hii.

Shukurani za pekee ninampa msimamizi wangu mpendwa Dkt. Hanna Simpassa, kwa kuutumia muda wake, kwa hali na mali katika kunitia moyo nilipoonekana kukata tamaa. Licha ya mapungufu niliyokuwa nayo aliweza kunivumilia, akaipitia kazi yangu, akaisahihisha na kunielekeza vilivyo ili kuhakikisha kuwa inakuwa inavyotakiwa kuwa. Mungu ambariki sana huyu mama! . Ninakishukuru Chuo Kikuu Huria cha Tanzania hasa Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii wakiwemo walimu wangu Dkt. Zelda Elisifa, Nestory Pembe Ligembe, Lipembe, Prof.Emmanuel Mbogo, James Mdee na Tigiti Sengo kwa taaluma, maarifa na ushauri walionipa na kwa ushirikiano mzuri ulioniwezesha kukamilisha kazi hii.Nasema asante sana,Mungu awajaalie mema.

Ninapenda kumshukuru sana mume wangu mpendwa Jonathan Joseph kwa kuniruhusu kujiunga na masomo na kunivumilia nilipokuwa mbali na familia yetu.Alijitwika mzigo wa kuikimu familia yetu katika kipindi chote cha masomo yangu.Mungu ambariki sana na kumshindia katika yote.Aidha, ninawashukuru sana watoto wetu wapendwa Tumaini Jonathan na Mercy Jonathan kwa kunivumilia kwani kipindi ambacho sikuwepo walikuwa wakikosa upendo wa mama.Naye wifi yangu Naomi Daniel tunayeishi naye.Mungu awabariki na kuwashindia katika masomo yao! Hakika wana kila sababu ya kufaulu.

Ninamshukuru mama yangu mpenzi Sussane Melkizedeck kwa kunishauri, kuniombea mafanikio na kunitia moyo mno katika safari ya masomo yangu haya.Baba yangu Ezekiel Nyanda pia hakuwa nyuma katika hili bila kuwasahau wapendwa dada yangu Consolata Nyanda na kaka zangu Andes Nyanda, Julius Nyanda na Edgar Nyanda, watoto wetu Ezekiel William na Suzan Nicholaus, wifi zangu Neema Mnuo na Sara Seni kwa ushauri wao na misaada ya hali na mali waliyonipa ili kuhakikisha kuwa ninafaulu.Wabarikiwe mno!

Siwasahau wanafunzi wenzangu tulioabiri nao chombo hiki kwa kunitia moyo na kunipa misaada yao ya hapa na pale.Nao ni Wenceslaus Mashaka, Nicholaus Lunyana, Reuben Luhende, Daud Mtega, January Magesa,Salome Mhangilwa, Deusdedit Omchamba na Angela Ghati. Nawashukuru na kuwatakia kila la heri, ushindi na mafanikio tele! Wafanyakazi wenzangu Alex Majenga na Josephine Msonsa, Wabarikiwe pia kwa misaada yao kwangu.

Ninajua kuna wengi waliochangia ambao sijawataja kwa ukosefu wa nafasi. Kwao wote ninasema asanteni sana na Mungu awabariki!.

# IKISIRI

Utafiti huu ulikuwa na lengo la kuchunguza Athari za Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili.Umetumia nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ili kuweka bayana athari hizo. Sura ya Kwanza imeshughulikia Utangulizi, Tatizo la Utafiti, Malengo ya Utafiti, Umuhimu wa Utafiti, Mawanda na Mipaka ya Utafiti na Mpango wa Utafiti.Sura ya Pili imeshughulikia Mapitio ya Kitaaluma na ya Kazi Tangulizi ambapo imeelezea yaliyoandikwa kuhusu lugha na athari za lugha za kibantu katika Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili.Aidha, imeelezea yaliyoandikwa kuhusu Ala za Sauti, Sauti za Lugha, Namna ya Utamkaji na Mahali pa Kutamkia Sauti za Kiswahili. Imeelezea Pengo la Maarifa na Kiunzi cha Nadharia. Sura ya Tatu imezungumzia Njia na Mbinu za Utafiti.Imezungumzia Utangulizi, Eneo la Utafiti, Sampuli ya Utafiti na Usampulishaji,Vyanzo vya Data,Ukusanyaji wa Data, Mkabala wa Uchambuzi wa Data,Uchambuzi wa Data na Vikwazo vya Utafiti.Sura ya Nne imeeleza juu ya Uwasilishaji na Uchambuzi wa data,ambapo imeelezea aina za fonimu za Kinyamwezi na Athari ya Lugha ya Kinyamwezi katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili. Sura ya tano imeeleza juu ya Muhtasari wa Utafiti na Mapendekezo.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ........ **ii**

**HAKI MILIKI** ........ **iii**

**TAMKO**………….. ........ **iv**

**TABARUKU** ........ **v**

**SHUKURANI** ........ **vi**

**IKISIRI**……….. ........ **viii**

**YALIYOMO** ........ **ix**

**VIELELEZO** ........ **xiii**

**SURA YA KWANZA** ........ **1**

**UTANGULIZI** ........ **1**

1.1 Utangulizi. ........ 1

1.1.1 Mada ya Utafiti ........ 1

1.1.1.1 Usuli wa mada. ........ 1

1.1.1.1.1 Lugha ya Kinyamwezi. ........ 1

1.1.1.1.2 Lugha ya Kiswahili. ........ 1

1.1.1.1.2 Mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti. ........ 2

1.2 Tatizo la utafiti. ........ 3

1.3 Malengo ya utafiti. ........ 3

1.3.1 Lengo kuu. ........ 3

1.3.2 Malengo mahsusi ........ 4

1.3.3 Maswali ya utafiti. ........ 4

1.4. Umuhimu wa utafiti. ........ 4

1.5 Mawanda na mipaka ya utafiti. ........ 6

1.6 Mpango wa utafiti. ........ 6

**SURA YA PILI.** ........ **7**

**MAPITIO YA KITAALUMA NA MAPITIO YA KAZI TANGULIZI. .............. 7**

2.1 Utangulizi ........................................................................................ 7

2.2 Mapitio ya Kitaaluma na Mapitio ya kazi tangulizi. ................................ 7

2.2.1 Yaliyoandikwa kuhusu lugha,Lugha ya asili,Lugha mama na Lugha ya Pili. ........................................................................................ 7

2.2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Uamiliaji lugha, Ujifunzaji lugha na Matumizi ya lugha ya Pili........................................................................................ 9

2.2.3 Yaliyoandikwa kuhusu athari za lugha za kibantu katika lugha ya Kiswahili. ........................................................................................ 16

2.2.4 Yaliyoandikwa kuhusu Ala za sauti, Sauti za Lugha, Namna ya utamkaji na Mahali pa kutamkia sauti za Kiswahili. .......................................... 18

2.2.4.1 Ala za sauti. ........................................................................................ 18

2.2.4.2 Fasili ya fonimu, Aina za fonimu za Kiswahili, Mahali pa kuzitamkia na Namna ya kuzitamka. ........................................................................ 19

2.2.4.2.1 Fasili ya fonimu........................................................................................ 19

2.2.4.2.2 Aina za fonimu za Kiswahili. ................................................................ 20

2.2.4.2.2.1 Fonimu za irabu/Vokali za Kiswahili sanifu........................................... 20

2.2.4.2.2.2 Fonimu za nusu irabu za Kiswahili sanifu /viyeyusho.......................... 23

2.2.5 Pengo la maarifa. ........................................................................................ 25

2.2.6 Kiunzi cha Nadharia. ................................................................................ 26

2.3 Hitimisho. ........................................................................................ 28

**SURA YA TATU ........................................................................................ 29**

**NJIA NA MBINU ZA UTAFITI................................................................ 29**

3.1 Utangulizi ........................................................................................ 29

3.2 Eneo la Utafiti. ........................................................................................ 29

3.3 Uteuzi wa Walengwa. ........................................................................ 30

3.3.1 Sampuli na Usampulishaji ... 30
3.4 Vyanzo vya Data. ... 32
3.4.1 Data za msingi. ... 32
3.4.2 Data za Upili ... 32
3.5 Ukusanyaji wa Data. ... 33
3.5.1 Vifaa vya kukusanyia Data. ... 33
3.5.2 Mbinu za ukusanyaji wa Data. ... 34
3.5.2.1 Mahojiano ... 34
3.5.2.2 Mbinu ya Hojaji. ... 35
3.5.2.3 Mbinu ya majadiliano ... 36
3.5.2.4 Maktabani (Mbinu ya kimaktaba). ... 37
3.6. Mkabala wa uchambuzi wa Data. ... 37
3.7 Uchambuzi wa Data. ... 38
3.8 Vikwazo vya Utafiti. ... 38
3.9 Hitimisho. ... 39
**SURA YA NNE ... 40**
**UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ... 40**
4.1 Utangulizi ... 40
4..2 Aina za fonimu za Kinyamwezi. ... 40
4.3 Athari ya Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili. ... 44
**SURA YA TANO ... 67**
5.1 Utangulizi. ... 67
5.2 Muhtasari wa Utafiti ... 67
5.3 Mchango wa Utafiti ... 68
5.4 Mapendekezo: ... 69

**MAREJELEO** ........................................................................................................ **71**

**VIAMBATANISHO**.................................................................................................. **74**

## VIELELEZO

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kielelezo na.2.1 | : | Jedwali la Irabu za Kiswahili Sanifu na Sifa Zake Bainifu …... | 22 |
| Kielelezo na.2.4 | : | Jedwali la Konsonanti na Nusu irabu za Kiswahili Sanifu…..... | 24 |
| Kielelezo na.3.1 | : | Jedwali la Mchanganuo wa Watafitiwa……………….……… | 31 |
| Kielelezo na.4.1 | : | Fonimu za irabu fupi za Kinyamwezi…………………….……... | 41 |
| Kielelezo na 4.2 | : | Fonimu za irabu ndefu za Kinyamwezi ………………………. | 41 |
| Kielelezo Na.4.3 | : | Matriki ya irabu za Kinyamwezi……………………………… | 42 |
| Kielelezo na.4.4: | : | Jedwali la Konsonanti na Nusu Irabu za Kinyamwezi………... | 43 |
| Kielelezo na. 4.5 | : | Jedwali la Watafitiwa Linaloonyesha Idadi na Majibu Yao… | 44 |
| Kielelezo Na.4.6 | : | Jedwali la Watafitiwa Linaloonyesha idadi na Majibu Yao….. | 45 |
| Kielelezo na.4.7 | : | Jedwali la Watafitiwa Linaloonyesha Idadi na Majibu Yao….. | 45 |
| Kielelezo na..4.8 | : | Jedwali la Watafitiwa Linaloonyesha Idadi na Majibu Yao….. | 46 |
| Kielelezo na.4.9 | : | Jedwali la Watafitiwa Linaloonyesha Idadi na Majibu Yao….. | 40 |
| Kielelezo na.4.10 | : | Jedwali la watafitiwa linaloonyesha idadi na majibu yao…….. | 48 |
| Kielelezo na.4.11 | : | Jedwali la watafitiwa linaloonyesha idadi na majibu yao…….. | 49 |
| Kielelezo na.4.12 | : | Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari katika matumizi ya /Ɵ/ ………………………………………………………….. | 50 |
| Kielelezo na.4.13 | : | Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari katika matumizi ya /ð/ ………………………………………………………... | |

51

Kielelezo na.4.14 : Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari katika matumizi ya /*b*/ ………………………………………………………….. 52

Kielelezo na.4.15 : Jedwali linaloonyesha mifano ya Uchopekaji wa silabi katika Neon…………………………………………………………… 53

Kielelezo na.4.16 : Jedwali linaloonyesha mifano ya Uchopekaji wa silabi katika Neon……………………………………………………………. 53

Kielelezo na.4.17 : Jedwali linaloonyesha mifano ya Uchopekaji wa sauti katika Neon………………………………………………….. 54

Kielelezo na.4.18 : Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari za kimaana………… 55

Kielelezo na.4.19 : Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari za kimaana………… 57

Kielelezo na.4.20 : Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari za kimaana………… 58

Kielelezo na..4.21 : Jedwali la Watafitiwa Linaloonyesha Idadi na Majibu yao…..... 63

Kielelezo na..4.22 : Jedwali la Watafitiwa Linaloonyesha Idadi na Majibu yao........ 63

Kielelezo na..4.23 : Jedwali la Watafitiwa Iinaloonyesha Idadi na Majibu yao...….. 64

## ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

[ ] Mabano ya fonimu.

/ / Mabano ya fonetiki.

TATAKI Taasisi ya Taalimu za Kiswahili.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi.

### 1.1.1 Mada ya Utafiti.

Athari za Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili.

#### 1.1.1.1 Usuli wa mada.

##### 1.1.1.1.1 Lugha ya Kinyamwezi.

Maendeleo ya lugha ya Kiswahili huchangiwa pia na lugha za kibantu, Kinyamwezi kikiwa miongoni mwazo. Kinyamwezi ni lugha ya kibantu nchini Tanzania inayozungumzwa na wanyamwezi. Mwaka wa 2006 idadi ya wasemaji wa Kinyamwezi imehesabiwa kuwa watu 980,000.

Kutokana na uainishaji wa lugha za Kibantu wa Malcom Guthrie Kinyamwezi kiko katika kundi la F20 na kinafanana na Kisukuma. Wanyamwezi ni kabila la Tanzania wanaoishi katika mikoa ya Tabora na Shinyanga.Lugha yao ni Kinyamwezi. Kukua kwa mji wa Tabora ambako ndiko kabila la Kinyamwezi liliko na kutokana na kuwa kituo kikubwa na kitovu cha biashara ya misafara ya watumwa, kulichangia sana Wanyamwezi kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano.

##### 1.1.1.1.2 Lugha ya Kiswahili.

Lugha ya Kiswahili ni lugha ya Kibantu ambayo chimbuko lake ni upwa wa Afrika Mashariki. Lugha hii iliainishwa na Guthrie (1948) kama lugha ya Kibantu ya kundi la G. (Polome, 1967; Mbaabu, 1991; Chimerah, 1998).

Kiswahili ni lugha ambayo awali ilianza kutumiwa na watu wachache walioishi katika mwambao wa Afrika Mashariki. Kwa wakati huo idadi ya watu hao ilikuwa ndogo. Leo hii lugha ya Kiswahili imekua na matumizi yake yameenea kwa haraka katika bara la Afrika, Ulaya, Marekani, Asia na Australia.

Ghanen (2005), anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha kubwa barani Afrika. Kwa ukubwa wake inafaa kabisa kuwa lugha ya kidiplomasia.Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika maswala kidiplomasia yatakifanya Kiswahili kuenea kwa kasi kubwa zaidi na kupata wazungumzaji wengi kuliko ilivyo leo. Nafasi ya lugha ya Kiswahili ni kule kupata fursa ya kuzungumzwa. Lugha hii huzungumzwa si tu Afrika Mashariki, Kati na Kusini bali hata ulimwenguni kiasi cha kufundishwa katika vyuo vikuu mbalimbali. Ni dhahiri kuwa Kiswahili kina nafasi ya kuwa miongoni mwa lugha zinazotambuliwa Afrika na duniani kwa ujumla. Hutumika pia katika umoja wa mataifa.

#### 1.1.1.1.2 Mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti.

Mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti husababisha kuathiriana kwa lugha hizo kutokana na kwamba kila lugha huchukua baadhi ya msamiati toka lugha nyingine na kuuingiza katika lugha yake.Lugha huathiriana na lugha nyingine endapo kutakuwa na mwingiliano baina ya wanajamii wa lugha hizo.Waongeaji wa lugha hizo wazungumzapo huwa kuna baadhi ya tofauti zinazojitokeza katika viwango vya kiisimu kuanzia fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Mwingiliano huu ulisababisha msamiati wa Kinyamwezi kuingia katika lugha ya Kiswahili. .

Masebo na Nyangwine (2008), wanaeleza kuwa lugha ya Kiswahili imeingiliana sana na lugha nyingine za Kibantu. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili ni ya pili katika jamii nyingi za kibantu, athari ya lugha ya kwanza inaonekana sana katika matamshi.Vilevile lugha za kibantu zimeathiri lugha ya Kiswahili katika maana, msamiati na sarufi.

**1.2 Tatizo la utafiti.**

Taasisi ya Elimu Tanzania (1996) inaeleza kuwa, Sarufi ni mfumo wa taratibu na kanuni zinazotawala matumizi sahihi ya matamshi ya maneno, maumbo ya maneno, miundo ya tungo na maana ya miundo.

Lugha ndicho chombo kikuu cha mawasiliano baina ya watu.Ili watu waweze kuitumia lugha kwa kuelewana, lazima kuwe na taratibu au sheria zinazotawala utumiaji wa lugha.Mzungumzaji akikiuka kanuni za lugha anazungumza lugha potofu. Taratibu za lugha hutawala matamshi ya maneno na vipengele vingine vya kisarufi.Watu hukosea kanuni za Kiswahili kutokana na athari za lugha za awali au lugha nyingine.Utafiti huu umelenga Kuchunguza Athari za Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Kiswahili.

**1.3 Malengo ya utafiti.**

Utafiti huu ulikuwa na malengo ya aina mbili, nayo ni lengo kuu na malengo mahsusi.

**1.3.1 Lengo kuu.**

Kuchunguza athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

### 1.3.2 Malengo mahsusi.

i). Kufafanua athari za lugha ya Kinyamwezi Kimsamiati, Kimatamshi na Kimaana katika kujifunza Kiswahili.

ii). Kubaini sababu zinazofanya lugha ya Kinyamwezi kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili Kimsamiati, Kimatamshi na Kimaana.

iii). Kubaini mbinu za kutumia ili kuwasaidia wanafunzi wanyamweziwanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili.

### 1.3.3 Maswali ya utafiti.

i) Ni athari zipi za Kimsamiati, Kimatamshi na Kimaana za Lugha ya Kinyamwezi zinajitokeza katika kujifunza lugha ya Kiswahili?.

ii) Zipi ni sababu za athari za lugha ya Kinyamwezi Kimsamiati, Kimatamshi na Kimaana katika kujifunza lugha ya Kiswahili?.

iii) Mbinu gani zitumike ili kuwasaidia wanafunzi wanyamwezi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili?.

## 1.4. Umuhimu wa utafiti.

Kufanyika kwa utafiti huu kumetoa mchango mkubwa wa kitaalamu, kinadharia na kiutamaduni.

Kwa upande wa taaluma, utafiti huu utapunguza pengo la kiutafiti juu ya athari za lugha ya Kinyamwezi katika lugha ya Kiswahili ambalo kwa ufahamu wa mtafiti, hakuna utafiti uliofanyika kwa kina juu ya mada hii. Hivyo utawasaidia wadau wa elimu kama vile wanafunzi, walimu, Maafisa Elimu kuwa na uelewa juu ya mada hiyo ya utafiti na hivyo kuweza kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa kufundisha lugha ya Kiswahili.

Matokeo ya uchunguzi huu ni ya manufaa kwa walimu watakaoyarejelea ili kutabiri uwezekano wa kutokea kwa makosa wakati wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wanaozungumza Kinyamwezi. Hivyo basi wataweza kuyatafutia ufumbuzi matatizo hayo kwa njia mwafaka.

Kupitia utafiti huu jamii itakuwa na ufahamu juu ya athari za Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili na hivyo kushirikiana kwa ukaribu na wadau wa elimu kuhamasisha uzungumzaji wa Kiswahili Sanifu. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ikiwa na ufahamu juu ya mada hiyo, itashirikiana na wakuza mitaala katika kuandaa mtaala wa elimu ambao utaridhia uzungumzaji wa lugha sanifu ya Kiswahili na uendelezaji wa lugha hiyo.

Utafiti huu utamsaidia mtafiti kama mwalimu, wanazuoni na wataalamu wa isimu kuelewa kwa undani zaidi juu ya athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili na hivyo kuielimisha jamii izitambue athari chanya na kisha kuchangia kukiendeleza Kiswahili , vilevile changamoto zitokanazo na athari hasi ili kuwawezesha kukabiliana nazo.

Utafiti huu utakuwa na utaendelea kuwa kichocheo cha tafiti nyingine kuhusu kuathiriana kwa lugha ya Kinyamwezi na Kiswahili katika jamii za Tanzania, Afrika na dunia nzima kwa ujumla.Utawasaidia watifiti wengine watakaoamua kufanya utafiti juu ya athari za lugha mama mbalimbali katika kujifunza Kiswahili na hivyo kuweka wazi njia nyingine mbalimbali za kuwasaidia wazawa wa lugha hiyo katika kujifunza lugha ya Kiswahili.Vilevile utakuwa rejea mojawapo kwa tafiti nyingine kuhusu isimu ya lugha.

Data zilizopatikana katika utafiti huu zitasaidia kutatua baadhi ya matatizo yaliyojitokeza na yatakayojitokeza katika tafiti nyingine zihusianazo na utafiti huu.

## 1.5 Mawanda na mipaka ya utafiti.

Lugha ya Kiswahili na Kinyamwezi ndizo zilizohusika katika utafiti huu ili kuchambua athari mbalimbali za Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili.Hii ina maana kwamba, mtafiti anafahamu kwamba lugha ya Kiswahili imeathiriwa na lugha kadhaa, lakini yeye alishughulikia athari ya Lugha ya Kinyamwezi peke yake katika kujifunza lugha ya Kiswahili kwani kama alivyokwishasema hapo juu , kwa ufahamu wake mada hii haikuwa imefanyiwa utafiti kwa kina.

## 1.6 Mpango wa utafiti.

Tasnifu hii ina jumla ya sura kuu tano zenye mada kuu na mada ndogondogo ndani yake.Sura ya kwanza inaelezea vipengele mbalimbali vya kiutangulizi.Sura ya pili inaelezea Mapitio ya kitaaluma na Mapitio ya kazi tangulizi huku Sura ya tatu ikiwasilisha Mbinu za utafiti.Sura ya nne imeelezea Uchambuzi wa data za utafiti na Sura ya tano ikitoa Muhtasari wa utafiti,Mchango wa utafiti,Mapendezo ya jumla, Mapendekezo ya tafiti zijazo na Hitimisho.

## 1.7 . Hitimisho.

Katika sura hii mambo yaliyozungumziwa ni Mada ya utafiti,Lugha ya Kinyamwezi,Lugha ya Kiswahili,Mwingiliano wa lugha mbili tofauti,Tatizo la utafiti,Malengo ya utafiti,Umuhimu wa utafiti,Mawanda na mipaka ya

# SURA YA PILI.

# MAPITIO YA KITAALUMA NA MAPITIO YA KAZI TANGULIZI.

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inajadili Mapitio ya kitaaluma na Mapitio ya kazi tangulizi. Marejeleo ya vitabu na Machapisho yanayohusiana na mada ya utafiti huu yamehusika. Sura hii inaonyesha mtazamo wa watalaam mbalimbali ulimwenguni kuhusiana na mada hii ya ya utafiti. Sehemu ya kwanza ya sura hii ni Utangulizi, inafuatiwa na sehemu ya pili, ambayo ni Mapitio ya kitaaluma na ya Kazi tangulizi  na sehemu ya mwisho ni Hitimisho. Aidha, Pengo la utafiti na Kiunzi cha nadharia vimeonyeshwa  ndani ya sehemu hii.

## 2.2 Mapitio ya Kitaaluma na Mapitio ya kazi tangulizi.

Katika sehemu hii Fasili ya lugha, Lugha ya asili, Lugha ya kwanza na Lugha ya pili, Uamiliaji lugha, Ujifunzaji lugha na Matumizi ya lugha ya Pili, Ala za sauti, Sauti za lugha, Namna ya utamkaji na Mahali  pa kutamkia sauti za Kiswahili, Pengo la maarifa na Kiunzi cha nadharia vimeelezewa.

### 2.2.1 Yaliyoandikwa kuhusu lugha,Lugha ya asili,Lugha mama na Lugha ya Pili.

Kabla ya kuongelea juu ya lugha fulani,ni jambo la muhimu kuelewa kwanza fasili ya lugha.Wataalam mbalimbali wameielezea lugha kwa namna zinazotofautiana kwa kiasi kidogo sana.Wafuatao ni miongoni mwa wataalamu hao.

Habwe  na Karanja  ( 2004 ), wakiinukuu TUKI (1990), wanasema kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu katika jamii wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana.Masamba na wenzake (2009), wanaeleza kuwa lugha ni

mfumo wa sauti nasibu ambazo zimebuniwa na jamii kwa madhumuni ya mawasiliano kati yao.

Hivyo basi, kulingana na maelezo ya wataalam hao, lugha ni mfumo wa sauti nasibu ambazo hutumiwa na watu wa jamii fulani wenye utamaduni unaofanana kwa madhumuni ya mawasiliano miongoni mwa jamii hiyo.

Msanjila na wenzake (2009), wanaeleza kuwa lugha ya asili ni lugha inayotokana na wanajamii wa eneo fulani ambao wana mila, desturi na utamaduni wa aina moja.Lugha ya asili huelezea mambo yahusuyo wanajamii hao kwa kina na kwa kujitosheleza.

Hivyo basi, lugha ya Kinyamwezi ni lugha inayotokana na wanajamii wa Tabora.Wanajamii hao ni Wanyamwezi ambao lugha yao ya asili ni Kinyamwezi.
Msanjila na wenzake (wameshatajwa), wanasema kuwa lugha mama ni lugha ya kwanza anayojifunza mtoto baada ya kuzaliwa. Masebo na Nyangwine (2008), wanaeleza kuwa lugha ya kwanza ni lugha ambayo mtu hujifunza utotoni mwake wakati anakua kabla hajaanza kujifunza lugha ya pili.Ni lugha ambayo mtoto hujifunza kwa kusikiliza kutoka kwa wazazi wake na majirani wanaomzunguka,kama wanazungumza lugha hiyo hiyo.Mtoto huigiza taratibu mpaka anapoufikia umilisi wa lugha ya kwanza (lugha mama).

Masebo na Nyangwine (2008), wanasema kuwa lugha ya pili ni lugha ambayo binadamu hujifunza baada ya kujifunza lugha ya kwanza. Kiswahili ni lugha ya pili kwa watu wengi wa Tanzania.

Msanjila na wenzake (wameishatajwa), wanaendelea kueleza kuwa lugha ya pili ni lugha anayojifunza mtu baada ya lugha yake ya kwanza au lugha mama. Kimsingi lugha ya pili huwa ni lugha rasmi inayotumiwa katika elimu, utawala na serikali. Kwa wazungumzaji wengine, lugha ya kwanza huwa pia ndio lugha ya pili kwa maana kwamba ndiyo lugha ya elimu, serikali na mawasiliano mapana. Hivyo basi, kwa wanyamwezi walio wengi lugha yao ya pili ni Kiswahili.

### 2.2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Uamiliaji lugha, Ujifunzaji lugha na Matumizi ya lugha ya Pili.

Binadamu anapozaliwa anakuwa na bohari la sauti mbalmbali zisizo na maana yoyote.Mara anapoanza kuishi katika jamii ndipo huanza kuibua sauti hizo katika mazingira bila mwenyewe kutarajia na kuanza kuzitafutia maana.

Wataalam mbalimbali wameongelea juu ya Uamiliaji lugha. Krashen na Tracy (1983), wanasema kuwa Uamiliaji lugha ni mchakato unaotokea katika nafsi iliyofichika akilini mwa mtu ambayo ndiyo imuongozayo kuongea au kuandika kwa urahisi.Hivyo wao wanaona kuwa uamiliaji hujitokeza kwa mtu katika hali ya ung’amuzi bwete pasipi mhusika mwenyewe kujitambua.

Jean (1992:123) anasema, katika uamiliaji lugha watoto wachanga wanakuwa makini katika lugha tangu wanapozaliwa.Wanaanza kutoa maneno yanayotambulika katika kipindi cha miezi 12 hadi 15 na kuanza kuyaunganisha maneno hayo kuanzia miezi 18. Anaendelea kusema kuwa watoto wote wasio na matatizo ya kimaumbile na baadhi wenye matatizo, wataanza kuongea ikiwa watasikia lugha ikizungumzwa katika mazingira waliyomo.

Massamba (2004), anasema kuwa, ujifunzaji lugha ni utaratibu wa kufanya jitihada rasmi za kuijua na kuitumia lugha fulani. Mtu yeyote ana uwezo wa kujifunza lugha na kuifahamu ikiwa tu atakuwa na akili timamu pamoja na alasauti zote zinazohusiana na ujifunzaji lugha. Kikubwa tu ziwe hazijaathiriwa au kuathirika.

Flyn (1984 -1987) kama alivyonukuliwa na Ellis (1996:453), kifaa cha uamiliaji lugha ya kwanza kitahusika na mchakato wa ujifunzaji lugha ya pili.Yeye anakubali kuwa Sarufi Majumui ni wezeshi katika ujifunzaji wa lugha ya pili kwani anaamini bado maarifa ambayo mjifunzaji wa lugha ya kwanza anayatumia katika ujifunzaji wa lugha hiyo ndiyo yale anayoyatumia mjifunzaji wa lugha ya pili. Waamiliaji wa lugha ya kwanza huwa na maarifa asilia ambayo huwawezesha kuiamili lugha yao kwa kutumia maarifa hayo.Sifa za mjifunzaji wa lugha ya kwanza ndizo anazokuwa nazo mjifunzaji wa lugha ya pili.

Jedwali lifuatalo linaonyesha baadhi ya tofauti zilizopo kati ya uamiliaji lugha na ujifunzaji lugha.

**KIELELEZO 2.1 : Jedwali linaloonyesha tofauti iliyopo kati ya Uamiliaji lugha na Ujifunzaji lugha:**

| NAMBA | UAMILIAJI LUGHA | UJIFUNZAJI LUGHA |
|---|---|---|
| 1. | Uamiliaji lugha hutangulia kisha kufuatiwa na ujifunzaji lugha.Yaani mtoto huanza kuzungumza pasipo kujua taratibu za lugha kama vile muundo na utamaduni wa lugha husika. | Ujifunzaji lugha hufuata baada ya uamiliaji lugha. Baada ya kujua kuzungumza ndipo hufundishwa sheria mbalimbali za lugha husika. |
| 2. | Hutokea katika ung’amuzi bwete yaani pasipo mtoto mwenyewe kujitambua kiakili, anajikuta tu ana uwezo wa kuzungumza vizuri bila kujua kwa nini anazungumza hivyo. | Ni tukio la kiutambuzi yaani mtu anajua fika kwamba anajifunza lugha. |
| 3. | Hapa huwa hahitajiki mtaalam wa lugha wala mazingira maalumu kama hayo. | Lazima kuwepo na mwalimu ambaye ni mtaalamu wa lugha pamoja na mazingira fulani ambayo yatamfanya yule mjifunzaji lugha kuweza kujifunza lugha kwa urahisi zaidi. |
| 4. | Si lazima kufuata sheria na kanuni za lugha au vipengele vya lugha. | Ni lazima mtu aelewe vipengele vyote vya lugha. |
| 5. | Utamaduni wa jamii husika hauzingatiwi sana. | Ni lazima mjifunzaji lugha aelewe na azingatie utamaduni wa jamii husika ili kuepuka makosa ambayo yanaweza kusababisha uhusiano mbaya na wanajamii husika. |

Tini wayo: [Chombozi.blogspot.com. 2013/11 (Ilisomwa tarehe 18.07.2014)].

Masebo na Nyangwine (wameishatajwa), wanaeleza kuwa, lugha ya pili ni lugha ambayo binadamu hujifunza baada ya kujifunza lugha ya kwanza. Kiswahili ni lugha ya pili kwa watu wengi wa Tanzania. Katika kujifunza lugha ya pili kunatawaliwa na vitu mbalimbali kama vile: walimu wanaofundisha, vifaa vya kufundishia.

Pamoja na maelezo yaliyotolewa na Masebo na Nyangwine (wameishatajwa) hapo juu kuhusu vitu vinavyotawala ujifunzaji wa lugha, jamii inayomzunguka anayejifunza lugha huutawala pia. Kwa mfano mtu anayejifunza Kiswahili akiwa hapa Tanzania na anayejifunza Kiswahili akiwa Zimbabwe, Ghana au Ureno, atakayekifahamu Kiswahili mapema ni yule ajifunzaye Kiswahili hicho akiwa Tanzania.

Tofauti kati ya mifumo-sauti ya lugha zinadhihirika zaidi wakati mtu anapojifunza lugha ya pili baada ya kuwa amekwishajua lugha yake ya mwanzo.Wakati huo, mfumo-sauti wa lugha yake umekwishaimarika kwa kiasi kikubwa na akijifunza lugha ya pili, mara nyingi anatafasiri sauti za lugha hii mpya kwa misingi ya fonolojia ya lugha yake ya kwanza.

Lugha ya pili hutumika katika kukidhi haja za mawasiliano na jamii ambazo siyo lugha yake ya kwanza. Hivyo kujifunza ni kwa lazima kwa lengo la mawasiliano.Vilevile ili kujihusisha na jamii inayozungumza lugha hiyo.

Kwa mujibu wa Chomsky (1976:29), Kama alivyonukuliwa na Ellis (1996:430), Sarufi Majumui ni mfumo wa kanuni na sheria ambazo ni msingi wa lugha za binadamu.Msingi wa nadharia hii ni kwamba binadamu anapozaliwa anakuwa na maarifa asilia ambayo humsaidia katika ujifunzaji wa lugha. Maarifa haya

hupatikana pale tu binadamu anapozaliwa kwani huwa na kifaa cha uamiliaji lugha ambacho kinakuwa na kanuni majumui na kanuni badilifu ambazo hukutana na tajiriba (uwezo wa jamii katika lugha) na kusababisha uamiliaji lugha kutokea.

Flyn (1984 -1987) kama alivyonukuliwa na Ellis (1996:453), kifaa cha uamiliaji lugha ya kwanza kitahusika na mchakato wa ujifunzaji lugha ya pili.Yeye anakubali kuwa Sarufi Majumui ni wezeshi katika ujifunzaji wa lugha ya pili kwani anaamini bado maarifa ambayo mjifunzaji wa lugha ya kwanza anayatumia katika ujifunzaji wa lugha hiyo ndiyo yale anayoyatumia mjifunzaji wa lugha ya pili. Waamiliaji wa lugha ya kwanza huwa na maarifa asilia ambayo huwawezesha kuiamili lugha yao kwa kutumia maarifa hayo.Sifa za mjifunzaji wa lugha ya kwanza ndizo anazokuwa nazo mjifunzaji wa lugha ya pili.

Ujifunzaji wa lugha ya pili hutokea katika miktadha mbalimbali tofauti.Wapo wanaojifunza lugha ya pili kwa urahisi sana kwa sababu katika mazingira ya nyumbani kwao kunatumika zaidi ya lugha moja ama lugha itumikayo nje ya nyumbani wanapokutana na wenzao kucheza, ni tofauti na ile ya nyumbani hali ambayo huwawezesha kujua lugha mbili au zaidi. Kwa wengine hili hutokea kwa sababu lugha moja au mbili hutumika na kufundishwa shuleni kwa muda mrefu. Hali hizi ndizo zimechangia upataji wa lugha ya Kiswahili kwani ni lugha ya pili kwa asilimia kubwa ya watumiaji wake. Hata baadhi ya Wanyamwezi, Kiswahili ni lugha ya pili kwao.

Kwa mujibu wa Gardiner (1985), na wafuasi wengine wa Saikolojia Jamii, mambo yanayochangia ujifunzaji wa lugha ya pili ni pamoja na umri, akili, kipaji, mielekeo ya lugha, muktadha wa kujifunza na matokeo ya kujifunza.

Gardiner (1985), anasema kuwa uamuzi wa kuendelea kujifunza na kuitumia lugha ya pili hutegemea sifa mbalimbali zinazohusiana na mielekeo na motisha.

Giles katika dibaji ya kitabu cha Gardiner ( 1985), anasema:

> "Kuna uwezekano wa tabia ya matumizi ya lugha kutegemea jinsi ambavyo wazungumzaji wanawakilisha tabia zao za kijamii na kisaikolojia, pamoja na jinsi, binafsi, wanavyoieleza hali husika kwa kuzingatia kaida na malengo yake……."Gardiner (ix ).

Corder (1967), anaeleza kuwa matatizo yajitokezayo mtu ajifunzapo lugha ya kwanza na lugha ya pili ni jambo la kawaida kutokea kabla ya mtumizi lugha kuzoea matumizi kamili ya kanuni za lugha ya pili. Kazi ya Selinker (1969), inaonyesha kuwa kuna mifanyiko mitano ya kisaikolojia ambayo ni muhimu katika kuchanganua matatizo katika matumizi ya lugha. Miongoni mwa mifanyiko hiyo kuna Ujumlishaji Mno Kiholela,Uhamishaji Lugha ambapo kanuni za lugha ya kwanza hutumiwa na hivyo kukiuka kanuni za lugha ya pili. Mikakati ya Mawasiliano Katika Lugha ya Pili, Njia za Kujifunza Zisizokuwa Halisi, na Uhamishaji wa Ufundishaji ambapo makosa kutokana na kutokuwa na umilisi kwa wanaofundisha.

Kila aina ya tatizo hudhihirika katika njia hizo zilizotajwa na Selinker. Kwa mujibu wake, makosa hayo huibua kiwango kingine katika matumizi ya lugha kinachoitwa Lugha – Kati yaani lugha inayojitokeza wakati mzungumzaji yuko katika harakati za kujifunza lugha ya pili kwani mzungumzaji wa lugha kati huhamisha kanuni za lugha ya kwanza na kuzitumia katika lugha lengwa.

Richard (1974) na Selinker (1972) wameorodhesha aina nne za makosa katika tungo. Mathalani:

a) Uhamishaji Lugha.

Huu ni utaratibu wa kuhamisha kiambajengo cha lugha moja na kukitumia katika lugha nyingine.Wanafunzi wengi huchukulia kuwa faridi za lugha ya kwanza na za lugha ya pili zinafanana.Vilevile, wanafunzi husadiki kuwa kanuni zinazotawala lugha mbili ni moja kwa hiyo zinaweza kutumiwa katika lugha zote mbili kwa njia ya kubadilishana.

b) Ufundishaji Mbaya wa Lugha ya Pili.

Ukosefu wa umilisi wa lugha ya pili, husababisha ufundishaji mbaya wa lugha ya pili. Baadhi ya walimu, aghalabu hukosa elimu mwafaka wajifunzapo lugha ya pili. Licha ya hayo baadhi walimu hukosa ujuzi wa kutosha katika lugha kwa kuwa baadhi yao hutumia mbinu zisizofaa zikiwemo ujumlishaji wa kiholela na pia matumizi mabaya ya sheria za lugha husika.

c) Mikakati ya Kuwasiliana Katika Lugha ya Pili.

Mawasiliano katika lugha ya pili hutokana na lugha mahsusi ambazo watu hujifunza ili kuweza kuwasiliana na wazungumzaji asilia wa lugha lengwa. Mara nyingi mwanafunzi hujaribu kadri awezavyo ili akabiliane na upungufu alionao katika lugha lengwa. Hivyo ili afikie mawasiliano bora iwezekanavyo, mwanafunzi huyo hujikakamua.

d) Ujumlishaji Mno Kiholela.

Ujumlishaji huu ni utoaji wa mahitimisho maelezo ya kijumla sana hadi kuvuka mpaka. Mara nyingi wanafunzi hutumia sheria kiholela yaani hata pasipofaa. Hivyo kutokana na kufanya hivyo wanafunzi hubaini chukulizi katika lugha lengwa na pia kuzitumia kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya pili na vilevile kusababisha makosa mengi katika lugha ya pili.

Selinker (1972), anawalaumu baadhi ya walimu wafundishao somo la lugha ya pili kama Kiswahili, ambao hutunia mbinu zisizofaa wanapofundisha. Krashen (1987) anaeleza kuwa kielelezo mwafaka cha ujifunzaji wa lugha kinahitajika. Aidha ameongeza kuwa mwalimu anafaa kuwa kielelezo bora katika matumizi ya lugha ya pili kama kilivyo Kiswahili Kwa wanafunzi wa Kinyamwezi.Walimu wanahimizwa kupiga msasa lugha yao maana makosa wanayoyafanya huigwa na wanafunzi wao.

Curtain (1990), anasisitiza kuwa mwalimu hafai kuathiriwa na lugha ya kwanza atamkapo maneno katika lugha ya pili.Wataalamu hawa wamependekeza kuwa matatizo ya walimu yasipuuzwe. Aidha, wanatakiwa kuwa kielelezo bora.

Brown (1993), anaeleza kuwa, matatizo ya wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili ni kuwa huwa hawatambui mfumo na kanuni za lugha husika.Wanafunzi wengi hukosa ujuzi katika lugha ya pili.Hivyo hawawezi kutambua makosa katika lugha hiyo.

### 2.2.3 Yaliyoandikwa kuhusu athari za lugha za kibantu katika lugha ya Kiswahili.

Lugha huathiriwa kutokana na matumizi ya watu, jinsi wanavyoitumia na kwa kiasi ambacho wameathiriwa na lugha yao ya kila siku. Wazungumzaji wa lugha nyingi za kikabila hapa nchini wameathiriwa na lugha zao za kwanza wakiwemo Wanyamwezi, ambapo wakati wa kuzungumza lugha ya Kiswahili hujikuta wameingiza kanuni na misingi ya lugha yao. Kitendo hiki huweza kuathiri lugha ya Kiswahili wakati wanapozungumza na pengine hata kupotosha ujumbe uliokusudiwa kwa msikilizaji.

Wanaisimu wamekuwa mstari wa mbele kubaini chanzo cha makosa na vilevile kubuni mbinu faafu zinazochangia katika kutatua matatizo hayo.Wataalam mbalimbali wamezungumzia swala hili, kwa mfano: Masebo na Nyangwine (2008),wanaeleza kuwa lugha ya Kiswahili imeingiliana sana na lugha nyingine za Kibantu. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili ni ya pili katika jamii nyingi za kibantu, athari ya lugha ya kwanza inaonekana sana katika matamshi

Massamba na wenzake (2001), wanaeleza kuwa wasemaji wa lugha mbili tofauti wanapokuwa na mawasiliano ya muda mrefu hawaachi kuathiriana kilugha. Lugha za kibantu pia zimekiathiri Kiswahili (Masebo na Nyangwine, 2003) wanaeleza kuwa, lugha za kibantu zimechangia asilimia 64 ya maneno ya Kiswahili.

Masebo na Nyangwine (2008), wanaeleza kuwa. Lugha ya Kiswahili imeingiliana sana na lugha nyingine za kibantu.Kwa kuwa lugha ya Kiswahili ni ya pili katika jamii nyingi za kibantu, athari ya lugha ya kwanza inaonekana sana katika matamshi. Vilevile lugha za kibantu zimeathiri lugha ya Kiswahili katika lafudhi, maana, msamiati na sarufi.Watu wengi wameathiriwa sana na lugha za kikabila wanapozungumza Kiswahili sanifu.

Ni kwa vipi Kinyamwezi kinaathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili ndilo swali kuu la utafiti huu. Chunguzi mbalimbali zimekuwa zikifanyika juu ya athari za lugha za kibantu katika lugha ya Kiswahili. Ingawa kumekuwa na juhudi za kuimarisha na kuboresha lugha ya Kiswahili,tafiti zinaonyesha kuwa wanafunzi wajifunzao lugha ya Kiswahili hufanya makosa katika mazungumzo yao. Baadhi ya makosa hayo yamo katika viwango vya Mofolojia, Fonolojia, Sintaksia na Semantiki.

Wanaisimu wamekuwa mstari wa mbele kubaini chanzo cha makosa na vilevile kubuni mbinu faafu zinazochangia katika kutatua matatizo hayo.Wataalam mbalimbali wamezungumzia swala hili, kwa mfano: Masebo na Nyangwine (2008),wanaeleza kuwa lugha ya Kiswahili imeingiliana sana na lugha nyingine za Kibantu. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili ni ya pili katika jamii nyingi za kibantu, athari ya lugha ya kwanza inaonekana sana katika matamshi.

Mara nyingi kama tutasikia mtu anaongea lugha yetu, na mara moja tukagundua kuwa ni mgeni wa lugha hiyo, sababu mojawapo inaweza kuwa, kwamba anakosea kuweka tofauti za kifonimu au kialofoni zinazohitajiwa, au anaingiza taratibu za fonolojia za lugha yake ambazo hazimo katika lugha anayojifunza. Hata lugha ambazo zina uhusiano wa kidugu zinaweza kutofautiana katika mifumo tofauti ya kifonolojia. Ni kwa vipi Kinyamwezi kinaathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili ndilo swali kuu la utafiti huu.

### 2.2.4 Yaliyoandikwa kuhusu Ala za sauti, Sauti za Lugha, Namna ya utamkaji na Mahali pa kutamkia sauti za Kiswahili.

#### 2.2.4.1 Ala za sauti.

Kila lugha huchagua baadhi tu ya sauti zinazoweza kutolewa na viungo-sauti vya mwanadamu.Na hata ikitokea kuwa kiuchunguzi lugha mbili zinatumia sauti zinazofanana,yaani zenye sifa sawa za kifonetiki zinaweza kutofautiana katika jinsi sauti zinavyotumika katika lugha hizo. Kwa hiyo ni kawaida kutarajia kuwa lugha zitakuwa na mifumo tofauti ya kifonolojia

Mgullu (2012), anaeleza kuwa, ala za matamshi ni vile viungo vya mwili wa mwanadamu ambavyo huhusika kwa namna moja au nyingine na utamkaji.Mtu anapozungumza hutumia viungo fulani.Viungo hivyo huhusishwa na uzungumzaji kwa viwango mbalimbali.Vingine huhusika sana, vingine wastani na vingine kidogo tu. Ala za matamshi hugawanywa katika makundi makuu mawili yaani:

(1) Ala sogezi (active speech organs).

(2) Ala tuli (passive speech organs).

Ala sogezi ni zile ala ambazo husogeasogea wakati mtu anapozungumza.Mifano yake ni **ulimi** na **midomo**. Ala tuli ni zile ambazo huwa zimetulia tu hazisogeisogei wakati mtu anapozungumza.Mifano mizuri ya ala tuli ni pamoja na **ufizi.**

Matinde (2012), anasema kuwa sauti za lugha ya mwanadamu hutamkwa pale ambapo viungo mbalimbali vya mwili wa binadamu hutatiza hewa inayoingia na kutoka mapafuni kupitia ama chemba ya pua au chemba ya kinywa.Viungo hivi vya mwili wa binadamu huitwa **ala za sauti**.

> Ala muhimu za matamshi ni *midomo, meno, ufizi, kaakaa gumu, kaakaa laini, kimio, ncha ya ulimi, bapa la ulimi, shina la ulimi, kidakatonge, nyuzi sauti, koo, pua, chemba ya pua, chemba ya kinywa na koromeo.*

### 2.2.4.2 Fasili ya fonimu, Aina za fonimu za Kiswahili, Mahali pa kuzitamkia na Namna ya kuzitamka.

#### 2.2.4.2.1 Fasili ya fonimu.

Mgullu (2012), anaeleza kuwa fonimu ni kipashio kidogo kabisa katika lugha kilicho na uamilifu wa kutofautisha maana katika maneno.

#### 2.2.4.2.2 Aina za fonimu za Kiswahili.

Mgullu ( 2001 ), Massamba na wenzake ( 2004 ) na Iribemwangi ( 2010 ) ni miongoni mwa wanaisimu walioushughulikia mfumo wa fonimu za Kiswahili. Hawa wameziainisha fonimu kama fonimu za irabu, fonimu za nusu irabu na fonimu za konsonanti.

Katika kuchunguza mifumo-sauti ya lugha mbalimbali, mfanano wa kifonetiki kati ya sauti ni muhimu sana, kama vile mahusiano yote ya kifonolojia, kanuni pamoja na minyumbuo yote. Katika kuainisha sauti za lugha, ili kugundua zipi ni fonimu za lugha hiyo pamoja na alofoni zake, umuhimu huwekwa katika kuangalia uhusiano uliopo kati ya makundi ya sauti kufuatana na mahali pa kutamkia na namna ya utamkaji.

Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004), wanaeleza kuwa, katika jedwali la IPA sauti za lugha zimeainishwa katika makundi mbalimbali kulingana na sifa zake bainifu.Kwa kutumia kigezo cha jinsi zinavyotamkwa, sauti za lugha zinagawanywa katika makundi mawili makuu:Konsonanti na vokali.

##### 2.2.4.2.2.1 Fonimu za irabu/Vokali za Kiswahili sanifu.

Habwe na Karanja (2004), wanasema kuwa vokali hutamkwa ala zikiwa zimeachana hivi kwamba hakuna mkwaruzo wazi kama wakati wa kutoa konsonanti.

Mgullu (2012), anaeleza kuwa, wakati wa kutamka irabu hewa huwa haizuiwi wala kubanwa mahali popote.

Kuna aina nyingi za irabu.Idadi ya irabu hutegemea lugha inayohusika kwani kila lugha huchagua idadi ya irabu kadhaa tu kutoka katika bohari la sauti..Jumla ya irabu za Kiswahili ni tano nazo ni / a /, /ɛ /, / i /, / ɔ / , / u /. Hizi ndizo huungana na konsonanti ili kuunda silabi. Irabu huainishwa kwa kutumia vigezo vitatu, navyo ni:

**i. Sehemu ya ulimi.**

Sehemu ya ulimi inayohusika wakati wa kutamka irabu inaweza kuwa ya mbele, kati au nyuma.Katika Kiswahili irabu za mbele ni na / i / na /ɛ / na ilhali zile za nyuma ni / ɔ / na / u / . Irabu ya kati ni / a /.

**ii. Mwinuko wa ulimi.**

Ulimi unaweza- kuinuliwa juu ukawa sambamba na sehemu ya juu ya kinywa

- kulazwa chini kinywani au
- kuwa katikati ya juu na chini ya kinywa.


a) Irabu zitamkwazo ulimi ukiwa umeinuliwa juu na sambamba na paa la kinywa ni za [+ juu], nazo ni / i / na / u /.
b) Irabu zitamkwazo ulimi ukiwa katikati ni /ɛ / na / ɔ / .
c) Irabu ambayo hutamkwa katika sehemu ya chini mwa kinywa ni / a /.
d) Irabu /ɛ / na / ɔ / zina sifa ya [-kaze] yaani zinapotamkwa ulimi hulegezwa ukilinganishwa na wakati wa kutamka / a /, / i / na / u / ambazo hutolewa ulimi ukiwa umekazwa.Sauti hizi huwa na sifa ya [+ kaze].

**iii. Mkao wa midomo**

Wakati wa utamkaji wa irabu mkao wa mdomo waweza kuwa mviringo au mtandazo. Irabu zinazotamkwa wakati mdomo ukiwa na mkao wa mviringo ni / u / na / ɔ /. Irabu zinazotamkwa wakati mdomo ukiwa na mkao wa mtandazo ni / a /, /ɛ / na / i / . Ikumbukwe kuwa kiwango cha mviringo au kutanda huwa tofauti

kulingana na irabu inayohusika. Mathalani mdomo hutanda wakati wa kutamka / a / zaidi ya /ε / na / i /. Mchoro ufuatao unaonyesha irabu zitamkwavyo:

**KIELELEZO 2.2 FONIMU ZA IRABU ZA KISWAHILI**




**Kielelezo 2.3 la irabu za Kiswahili sanifu na sifa zake bainifu.**

| | /a / | / ε / | / i / | / ɔ / | / u / |
|---|---|---|---|---|---|
| Juu | - | - | + | - | + |
| Chini | + | - | - | - | - |
| Nyuma | - | - | - | + | + |
| Mbele | - | + | + | - | - |
| Mviringo | - | - | - | + | + |
| Kaze | + | - | + | - | + |
| Kati | + | - | - | - | - |

Kwenye jedwali hili tunaona kuwa irabu ambazo ni [+juu] na [+nyuma] zina sifa za [+mviringo]. Hivyo / u / ambayo ni sauti ya [+juu] na pia [+nyuma] ina sifa ya [+mviringo].Vilevile ,sauti za [-nyuma] na [-juu] ni [-mviringo].Sauti hizo ni /a /

na / ε /.Vivyo hivyo,sauti za [- chini] na [-nyuma] ni [+mbele] nazo ni / ε / na / i / . Sauti za [-chini] na [-juu] ni [-kaze]. / a / pekee ndiyo [+kati].

#### 2.2.4.2.2.2 Fonimu za nusu irabu za Kiswahili sanifu /viyeyusho.

Fonimu za nusu irabu ni / w / na / j /.Sauti hizi hutamkwa kwa kuachilia hewa kutoka katika mapafu kupitia kinywani au kwenye mkondo hewa wa pua kwa mkwaruzo mdogo. / w / hutamkwa mdomo ukiwa na mkao wa mviringo na shina la ulimi limevutwa nyuma kuelekea kwenye kaakaa laini. / j / hutamkwa midomo ikiwa imetanda huku bapa la ulimi likiwa limeinuliwa kuelekea kaakaa gumu.Kwa mujibu wa Iribemwangi (2010), sauti hizi hudhihirika wazi katika mifanyiko ya kifonolojia,hasa uyeyushaji.

#### 2.2.4.2.2.3 Fonimu za konsonanti za Kiswahili sanifu.

Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa, konsonanti ni sauti ya lugha inayotamkwa wakati ambapo hewa kutoka mapafuni huzuiliwa kabisa au kidogo hivi kwamba nafasi ya hewa ni ndogo sana kiasi cha hewa kupita kwa mkwaruzo.Mradi konsonanti hupita kwa mkwaruzo wa namna fulani.Sifa bainifu ambazo hutumiwa katika kubainisha konsonanti ni:

i. mahala pa kutamkwa
ii. namna ya kutamka.

Idadi ya Konsonanti za Kiswahili sanifu hutajwa tofautitofauti na wataalamu mbalimbali.Kwa mfano Mgullu (2001) na Polome ( 1967) wameorodhesha konsonanti 24,Massamba na wenzake (2004), wameainisha Konsonanti 23 na Iribemwangi ( 2010) ameorodhesha konsonanti 25. Utafiti huu utatumia idadi ya konsonanti 25 zilizogawanywa katika makundi sita makuu.Makundi hayo ni Vizuiwa

( */p/, /b/, /t/, /d/, /k/, /g/*), Vikwamizwa ( */s/, /z/, /f/, /v/, /Ɵ/, /ð/,/ ʃ /, /x/, / γ /, /h/),*

Vizuiwa Kwamizwa *( /ts/, / ɟ / )* Nazali *(/m/, / ɱ / /n/, / ŋ /, / ɲ /)*, Kitambaza ( */l/* )

na Kimadende *(/ r/ )*.

**KIELELEZO 2.4 JEDWALI LA KONSONANTI NA NUSU IRABU ZA KISWAHILI.**

| **NAMNA YA KTAMKA** | **MAHALI PA KUTAMKWA** | | | | | | | | **HALI YA GLOTA** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vizuiwa/ Vipasuo | Midomo | Midomo na Meno | Meno | Ufizi | Kaaka Gumu na Ufizi | Kaakaa Gumu | Kaakaa Laini | Koromeo | |
| | b | | | d | | | g | | Ghuna |
| | P | | | t | | | k | | Hafifu |
| Vizuiwa Kwamizwa | | | | | | / ɟ / | | | Ghuna |
| | | | | | | / ʧ / | | | Hafifu |
| Vikwa-Mizwa | | v | ð | z | | | γ | h | Ghuna |
| | | f | Ɵ | s | ʃ | | x | | Hafifu |
| Nazali | m | ɱ | | n | | ɲ | ŋ | | Ghuna |
| Kitambaza | | | | l | | | | | Ghuna |
| Kimadende | | | | r | | | | | Ghuna |
| Nusu Irabu | w | | | | | y | | | Ghuna |

### 2.2.5 Pengo la maarifa.

Chunguzi mbalimbali zimekuwa zikifanyika juu ya athari za lugha za kibantu katika lugha ya Kiswahili. . Ingawa kumekuwa na juhudi za kuimarisha na kuboresha lugha ya Kiswahili,tafiti zinaonyesha kuwa wanafunzi wajifunzao lugha ya Kiswahili hufanya makosa katika mazungumzo yao. Baadhi ya makosa hayo yamo katika viwango vya Mofolojia, Fonolojia, Sintaksia na Semantiki. Wanaisimu wamekuwa mstari wa mbele kubaini chanzo cha makosa na vilevile kubuni mbinu faafu zinazochangia katika kutatua matatizo hayo.

Corder (1967), anasema kuwa makosa katika lugha ya pili yanaonyesha hali fulani ya matatizo aliyonayo mzungumzaji katika lugha ya pili kutokana na kuhamisha sifa fulani za lugha ya kwanza hadi kwenye lugha ya pili.

Maelezo ya Onyango (1997), Ndung'u (1999) na Mutugu (2001) yanathibitisha kuwa watumiaji wengi wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili hukumbwa na matatizo wakati waitumiapo kama lugha ya pili. Kujitokeza kwa makosa hayo huwa katika viwango vya kifonolojia, mofolojia na hata sintaksia.

Otiende (2014),alifanya utafiti juu ya **'Athari za Kimofofonolojia za Kiolosuba Katika Matumizi ya Kiswahili Kama Lugha ya Pili'**. Obara (2014), alitafiti juu ya **'Uchanganuzi wa Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi Wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii'**. Mbula (2011), alichunguza '**Makosa ya Kifonolojia Yanayofanywa na Wazungumzaji wa Kikamba Wanapozungumza Kiswahili Sanifu**.'William (2013), alichunguza **'Athari za Sheng Kwa Lugha ya Kiswahili'**. Vilevile Kisakwa (2014), katika tasnifu yake kuhusu '**Uchanganuzi wa Makosa na Muundo Sentensi: Ulinganisho wa Sentensi Sahili za Kiswahili'**, anaeleza kuwa

wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili hufanya makosa mengi yakiwamo matamshi mabaya ya maneno. Katika utafiti wake alibaini kuwa makosa mengi hujitokeza katika tungo za wanafunzi na kuwa makosa hujidhihirisha katika vipashio vyote vya lugha ijapokuwa kwa asilimia tofauti.

Lusesa (2013), alichunguza **'Athari za Lugha ya Kisukuma Katika Kujifunza Kiswahili'**. Huyu alisema kuwa kuna haja ya kufanya tafiti za kina zaidi za kubainisha athari za lugha za kibantu katika kujifunza Kiswahili na mbinu za kuwasaidia wazungumzaji wa lugha mama za kibantu wanaojifunza lugha ya Kiswahili.

Ingawa Maganga na Schadeberg (1992) katika kitabu chao waliandika juu ya sarufi, matini na msamiati wa Kinyamwezi, hawakueleza juu ya athari za lugha hiyo katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Kwa upeo wa ufahamu wa mtafiti hakuna mtafiti aliyewahi kujishughulisha kuhusu athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza Kiswahili. Hivyo mtafiti anakubali kuwa ni muhimu kuendeleza utafiti kuhusu athari za lugha za kibantu katika kujifunza Kiswahili Hivyo basi, ili kuziba pengo hilo Utafiti huu umelenga kuongeza mchango huo kwa kuchunguza '*Athari za Kinyamwezi katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili'*.

### 2.2.6 Kiunzi cha nadharia.

Ili utafiti kufanya utafiti ufanyike kwa uaminifu na uthabiti wenye kuzaa matunda tarajiwa kulingana na lengo la utafiti huo,ni lazima utafiti huo uongozwe na nadharia sahihi kwani nadharia hiyo hubeba mawazo,dhana au maelezo yatolewayo kwa nia au kwa lengo la kueleza hali fulani, Chanzo, muundo au utendaji wa jambo.

Mdee na wenzake,(2011),wanaeleza kuwa nadharia ni mpango wa mawazo uliotungwa ili kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani.Massamba (2004:63), kama alivyonukuliwa na Msanjila (2006:42), anasema kuwa, nadharia ni utaratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumika kama kielelezo cha kuelezea jambo.

Hivyo basi, kwa kuwa nadharia ni dira na mwongozo,utafiti huu utaongozwa na nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia.Vennemann ndiye aliyeiasisi nadharia hii katika kutoa udhahania ulioonekana katika Fonolojia Zalishi. Licha ya hilo, Hooper (1971) ndiye aliyeiendeleza katika tasnifu yake iliyoitwa``Aspects of Generative Phonology. Mwaka 1979 kazi hii ilichapishwa kwa kichwa cha Introduction to Natural Generative Phonology. Kwa mujibu wa Massamba (2012), nadharia hii iliwavutia wanazuoni wengi kuliko ilivyokuwa kwa Fonolojia Asilia. Massamba 1996:160), anaeleza kuwa Fonolojia Asilia Zalishi ni mkabala. Hivyo ni wazi kabisa kuwa matatizo ya Fonolojia Zalishi ndiyo yaliyoifanya Fonolojia Zalishi Asilia izuke ili kujaribu kuyatatua. Nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia huchunguza maumbo ya ndani ya maneno ili kupunguza udhahania.. Hivyo humwezesha mchunguzi wa lugha kufikia utabiri sahihi kuhusu Lugha Asilia, Hooper anaita jambo hili Kanuni ya Ujumulishaji Sahihi.Kanuni hii inawasilisha uhusiano kati ya miundo nje na kanuni za jumla kauli za kijumla ambazo lazima zidhihirike kama za kweli katika kila neno husika.

Kwa mujibu wa Hooper (1975), madai ya msingi katika Fonolojia Zalishi Asilia ni kwamba, “Katika usemaji wao, wasemaji wa lugha hutunga majumuisho ambayo yanadhihirika katika kinachotamkwa na kuleta uangavu wa kilichokusudiwa’’.Usemaji huu unaashiria kwamba majumuisho ambayo

hayadhihiriki katika utamkaji na ambayo hayaleti uangavu wa kitu kilichokusudiwa kusemwa, si halisi .

Hooper (1976), anaeleza kwamba lengo la wananadharia wa Isimu ni kuvumbua nadharia iliyo na uwezo wa kueleza maswala kuhusu lugha asilia lakini sio kuwa na nguvu kuliko kutumika katika lugha asilia.Miongoni mwa vipengele vilivyojadiliwa na Hooper ni kipengele cha Upataji Lugha. Massamba (ameishatajwa), anaeleza kuwa Hooper, akiwa anaunga mkono maoni ya Vennemann (1972a), anadai kwamba katika lugha kuna kategoria ambazo hujifunzwa kwanza; kwamba kutokana na kategoria hizo kunaweza kuongezewa mambo mengine au kufanyiwa marekebisho fulani, iwapo lazima; na kwamba hayo marekebisho yanayofanywa, yanayobadilishwa au yanayoongezewa ndiyo yanayotupa kategoria za upili. Massamba anaendelea kusema kuwa Fonolojia Zalishi Asilia ilijikita katika kuonyesha kuwa ingawa fonolojia ilikuwa zalishi lakini, uzalishi wake ulikitwa katika uasilia wa maneno yaliyokuwa yakitolewa na maumbile ya binadamu yanayohusu usemaji. Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kwamba nadharia hii ni muafaka katika kuelezea athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza Kiswahili; kwani inajihusisha na namna maneno yanavyotamkwa.

## 2.3 Hitimisho.

Katika sura hii tumeona mapitio mbalimbali ya kitaaluma na ya kazi tangulizi. Sura hii inaonyesha mtazamo wa watalaam mbalimbali ulimwenguni kuhusiana na mada ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza ya sura hii ni utangulizi, inafuatiwa na sehemu ya pili, ambayo ni mapitio kitaaluma na ya kazi tangulizi na sehemu ya mwisho ni hitimisho. Aidha, Pengo la utafiti na kiunzi cha nadharia vimeonyeshwa ndani ya sehemu hii. Sura inayofuata inahusu njia na mbinu za utafiti.

# SURA YA TATU

# NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sehemu hii inaelezea Mpango wa utafiti, Eneo la utafiti, Sampuli ya utafiti na Usampulishaji, Vyanzo vya data, Usanifu wa utafiti , Ukusanyaji wa Data, Mkabala wa Uchambuzi wa Data, Uchambuzi wa Data na Vikwazo vya Utafiti. Kent (1978), anasema kuwa, utafiti ni njia, au taratibu ya kufikia ujuzi na maarifa. Kazi hii ya utafiti ni kazi inayochunguza data na kueleza jinsi ilivyo.Kothari (2008), anasema kwamba, utafiti ni nyenzo muhimu inayosaidia kufahamu tabia, mahusiano na mwenendo wa makundi mbalimbali ya wanajamii na sehemu mbalimbali duniani. Utafiti wa aina hii huitwa utafiti wa sayansi jamii.

## 3.2 Eneo la utafiti.

Kabla ya kukusanya data za Utafiti ni jambo la busara kuchagua mahali ambapo upatikanaji wa data utatosheleza majibu ya maswali ya utafiti na hivyo kufanikisha lengo la utafiti.Ngure, (2011:198), anaeleza kwamba inabidi kuamua ni wapi utakusanya data unayohitaji.

Uchunguzi ulijikita katika Mkoa wa **Tabora,**Wilaya ya **Urambo** katika kata mbili ambazo ni **Urambo** *( Ukombozi Shule ya Sekondari* na *shule za Msingi Azimio,Ukombozi,Mwenge na mabatini)* *na* **Michikichini** *(Chetu shule ya Sekondari).*Wilaya hii ni miongoni mwa wilaya za Mkoa wa Tabora nchini Tanzania. Mtafiti aliteua kata hizo mbili tu moja ikiwa ya mjini na nyingine ya nje ya mji kwani mazingira ya maeneo hayo waliyomo watafitiwa yalikuwa na sifa toshelevu za kuwezesha kupatikana kwa majibu ya maswali ya utafiti.

### 3.3. Uteuzi wa walengwa.

Katika utafiti huu kundi lengwa lilikuwa ni wazungumzaji na wataalamu wa lugha ya Kiswahili na Kinyamwezi.Walliman (2011),anafafanua kundi lengwa kuwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika utafiti(vinavyotafitiwa)yaaniwatu taasisi vitu au matukio.Kwa ujumla,kundi lengwa ni jumla ya walengwa wote wa utafiti ambapo sampuli inaweza kuchaguliwa.

Kothari (2004:55), anaelezea kuwa, uteuzi wa walengwa ni mbinu au utaratibu ambao mtafiti atatumia katika kuchagua orodha ya vitu au watu kwa ajili ya sampuli. Walengwa wa utafiti huu hugawanywa katika makundi mawili, kundi la kwanza ni jamii ya kutafitiwa na kundi la pili ni sampuli itakayoshungulikiwa.

Copper (1989) na Vans (1990) wanasema kuwa, kundi lengwa ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake.

### 3.3.1 Sampuli na usampulishaji

Mtafiti aliwateua sampuli ya utafiti kulingana na sifa kuwa wana uwezo wa kutoa data sahihi zinazotakiwa kulingana na lengo la utafiti huu yaani waliokuwa na uwezo wa kutoa habari faafu zilizojibu kikamilifu maswali ya utafiti.

Babbie (1992), anasema kwamba, Sampuli ni sehemu ya idadi ya watu ambayo mtafiti anavutiwa nayo katika kupata taarifa na kutoa hitimisho la utafiti wake. Sigh (2007),usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa

Katika utafiti huu watafitiwa 40 waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa, nasibu na tajwa. Miongoni mwao, watafitiwa 08 walikuwa walimu wa Shule ya Sekondari na Msingi waliokuwa wakifundisha somo la Kiswahili ambao waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa (wa kimakusudi). Watafitiwa 23 walikuwa wanafunzi wa shule 02 za Sekondari Wanyamwezi wazawa waliokuwa wakijifunza somo la kiswahili ambao waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji nasibu na tajwa. Watafitiwa 09 walikuwa wamilisi wazawa wa lugha ya Kinyamwezi wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili waliokuwa na umri kati ya miaka 45 hadi 80 wakiwemo wazee mashuhuri na magwiji wa Kiswahili na Kinyamwezi,hawa waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa na tajwa. Mtafiti aliamua kutumia aina hizi za sampuli katika utafiti wake kwa sababu aliamini kuwa makundi hayo ndiyo yaliyokuwa na uwezo wa kutoa taarifa faafu.Mgawanyo wa sampuli hiyo inwasilishwa ifuatavyo:

**KIELELEZO 3 1 : Jedwali la mchanganuo wa watafitiwa:**

| **Namba** | **Makundi ya watafitiwa** | **Idadi ya watafitiwa Iliyotarajiwa** |
|---|---|---|
| 1. | Walimu waliokuwa wakifundisha somo la Kiswahili Shule ya Msingi na Sekondari. | 08 |
| 2. | Wanafunzi wa sekondari Wanyamwezi waliokuwa wakijifunza Kiswahili. | 23 |
| 3. | Wamilisi wa lugha ya Kinyamwezi walookuwa wakizungumza lugha ya Kiswahili. | 09 |
| Jumla | | 40 |

### 3.4 Vyanzo vya data.

Muligo (2012), anasema kwamba kuna aina kuu mbili za data, nazo ni data za msingi na data za upili.

#### 3.4.1 Data za msingi.

Data za msingi ni data halisi ambazo zilikusanywa na mtafiti kwa mara ya kwanza. Kufanya utafiti maskanini kulimwezesha mtafiti kukusanya data mbalimbali zilizohusu mada ya utafiti katika maskani mbalimbali.

Berg (2007), anasema kuwa maskani ni mahali ambapo watu wanaishi na mtafiti anapokwenda kutafuta kupata data ambazo ni mpya halisi ghafi ambazo kwanza hazikuwahi kukusanywa na mtu mwingine yeyote kwa ajili ya utafiti kama wake. Katika utafutaji na ukusanyaji wa data, mtafiti alikutana na walimu, wanafunzi na wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kinyamwezi.

#### 3.4.2 Data za upili .

Data za upili katika utafiti huu zilipatikana kwa kusoma vitabu na machapisho mbalimbali. Maandishi mbalimbali yalipitiwa maktabani, ikiwa ni pamoja na vitabu, makala, majarida na kwenye mtandao wa mawasiliano ili kupata mwelekeo muafaka kuhusu mada ya utafiti na hivyo kumwongoza mtafiti katika uchunguzi wake. Tafiti tangulizi zimesomwa ili kupata mwangaza kuhusu nadharia, mbinu za ukusanyaji data, uwasilishaji, na uchanganuzi wa matokeo ya utafiti.

Ewan na Calvert (2000), wanasema kwamba, maktaba ni mahali maalumu palipohifadhiwa nyaraka, vitabu, majarida, magazeti yenye taarifa mbalimbali kwa wasomaji na utafiti wa kada tofauti tofauti za taalam.

Maktaba zilizotumika katika utafiti huu ni za Mkoa wa Mwanza na ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Mbinu ya kujisomea pia ilimwezesha mtafiti kusoma makala, majarida na vitabu vilivyosaidia kuelezea athari za Kinyamwezi katika Kiswahili.

### 3.5 Ukusanyaji wa data.

Katika utafiti huu taarifa mbalimbali zilikusanywa kutoka maktabani na uwandani kwa kutumia mbinu na vifaa mbalimbali vilivyoandaliwa na mtafiti. (Kombo na Tromp 2006),wanaeleza kuwa,ukusanyaji wa data unahusu kukusanya taarifa mahsusi zilizokusudiwa kutoa au kupinga uhalisia wa mambo fulani (Kombo na Tromp 2006).

#### 3.5.1 Vifaa vya kukusanyia data.

Mtafiti aliandaa vifaa vya utafiti kulingana na mada na malengo ya utafiti. Vifaa hivi vilimwezesha mtafiti kukusanya data husika na kupata taarifa sahihi za utafiti wake.

i. **Shajara:** Kifaa hiki kilimsaidia mtafiti katika kunukuu na kuhifadhi baadhi ya data za msingi kama vile tarehe, majina ya wahojiwa, mahali pa wahojiwa,data za msingi na data fuatizi katika utafiti huu.

ii. **Kinasa Sauti:** Kifaa hiki kilitumika katika kunasa na kurekodi sauti wakati wowote katika miktadha mbalimbali hivyo mtafiti alikitumia kurekodi mahojiano baina yake na watafitiwa. Taarifa zilizorekodiwa zilitumika katika uchambuzi wa data katika utafiti huu.

iii. **Kompyuta:** Ilitumika katika kutafutia matini kutoka katika tovuti na wavuti na pia kuhifadhi taarifa mbalimbali. Data zilizohifadhiwa zilichambuliwa na kutolewa mahitimisho kisha kutumika katika kuandaa ripoti ya utafiti. Pia kompyuta ilitumika kama sehemu ya maktaba tembezi.

iv. **Kinyonyi:**Hiki kilitumika kuhifadhia data mbalimbali.

### 3.5.2 Mbinu za ukusanyaji wa data.

Mtafiti anatakiwa kuteua kwa makini Mbinu za ukusanyaji wa data ambazo zikitumiwa ipasavyo zitawezesha kufanikiwa kwa lengo lililokusudiwa na Mtafiti. Kothari (1990), anasema kwamba ukusanyaji data ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti.

Vile vile Kothari (ameishatajwa), anaendelea kusema kuwa hatua ya uwasilishaji na uchanganuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji data.Msaghaa (2010) anasisitiza kuhakikisha kuwa njia/mbinu za utafiti zinatoa aina ya taarifa zinazohitajika kujibu swali la utafiti.

Mtafiti alitumia mbinu ya hojaji, mahojiano, na majadiliano.Vilevile mbinu ya kimaktaba ambayo ilitumika kwa kusoma vitabu na makala zilizohusiana na athari za lugha na jinsi zilivyoathiri lugha ya Kiswahili. Mbinu hizi za ukusanyaji wa data zilimsaidia mtafiti kukusanya taarifa za kutosha katika utafiti.

#### 3.5.2.1 Mahojiano.

Mahojiano haya yalifanywa baina ya mtafiti na wahojiwa. Mbinu hii ilihusisha uwasilishaji wa maswali kwa wasailiwa wa maswali hayo ambayo yalijibiwa kwa njia ya mdomo na mtafiti alirekodi majibu hayo na kuandika katika shajara.

Kothari (2004:97), anasema kuwa, njia hii hutumika kukusanya data na huwasilishwa kwa njia ya mdomo ana kwa ana baina ya mtafiti na mtafitiwa. Kwa hiyo mtafiti alitumia mahojiano ya siri na wazi katika ukusanyaji wa data. Maswali funge yalitumiwa ambapo zilihitajika data au taarifa maalumu, huku maswali ya

sifunge yakitumiwa kumpa mtafitiwa nafasi ya kutosha kujieleza awezavyo juu ya mambo yaliyohusiana na mada ya utafiti Hii ni njia ya kupata data kwa kutumia maswali na majibu yanayofanywa kwa mazungumzo kati ya mtafiti na mtafitiwa (Kothari 2008).

Mbinu hii ni ya madhubuti katika kumpatia Mtafiti data za kutosha kujibu maswali ya utafiti wake kwa muda mfupi.(Borg na Gall,2003).Kothari (ameishatajwa), anaendelea kusema kuwa mbinu hii inaruhusu mtafiti kuuliza maswali ya ziada.

Mbinu hii ilimwezesha Mtafiti kupata data ambazo hapo awali hakutegemea kuzipata.Aidha,mbinu hii ilimwezesha Mtafiti  kuuliza maswali ya ziada na kufafanua ipasavyo maswali ambayo hayakueleweka kwa watafitiwa.Hali kadhalika mtafitiwa alipata nafasi ya kufafanua majibu au kumtaka Mtafiti kuliweka wazi swali ambalo halikueleweka ipasavyo kwa Mtafitiwa. Data zingine alizikusanya kutoka kwa wasiojua kuongea Kiswahili fasaha na sanifu na wengine walikuwa hawajui kusoma na kuandika.

Hata hivyo,mapungufu ya mbinu hii ni kwamba Mtafiti hawezi kupata data kutoka kwa watafitiwa wengi kwa muda mfupi.Mapungufu ya mbinu hii yalitatuliwa na matumizi ya hojaji.

**3.5.2.2 Mbinu ya hojaji.**

Katika utafiti huu, mbinu hii ilisaidia katika kukusanya data ambazo mtafiti alizipata kutoka kwa wataalamu wa lugha katika maeneo yote mawili. Ilimsaidia mtafiti kukusanya data kwani aliwapatia maswali wahojiwa katika maeneo husika kulingana na malengo ya utafiti .

Baraza la Kiswahili la Zanzibar (2010), linaeleza kuwa, hojaji ni karatasi ya maswali ya utafiti kuhusu jambo maalumu.Kwa mujibu wa Kothari (1990), mbinu ya hojaji ni mbinu ya utafiti ambayo kwayo mtafiti huandaa maswali kuhusiana na jambo fulani.Maswali hayo yanaweza kuhitaji majibu marefu au mafupi kutegemeana na taarifa inayohitajika na mtu anayepewa maswali hayo.

Kulingana na maelezo ya wataalam hao, hojaji ni maswali yaliyoandaliwa na mtafiti kwa lengo la kumhoji mtafitiwa, na maswali haya yanafungamana na malengo ya utafiti husika.Mbinu hii ilimwezesha Mtafiti kukusanya data nyingi kwa muda mfupi kutoka kwa watafitiwa wengi tofauti na ilivyokuwa katika mbinu ya usaili.Ilimwezesha Mtafiti kuutumia muda wake vizuri kwani wakati watafitiwa walipokuwa wakijaza hojaji yeye alikuwa akiendelea na shughuli nyingine.Hata hivyo,mbinu hii ina mapungufu kwani haikuweza kutumika kwa watafitiwa wasiojua kusoma na kuandika.Upungufu huu ulitatuliwa na mbinu ya mahojiano.

### 3.5.2.3 Mbinu ya majadiliano.

Njia hii ilitoa nafasi kwa Mtafiti na mtafitiwa kubadilishana mawazo.Hivyo ilisaidia mtafitiwa kutoa haraka taarifa au habari nyingi nzuri za kufaa.

Kwa mujibu wa TATAKI (2013: 300), Majadiliano, ni mazungumzo ya watu wawili au zaidi wanaobadilishana mawazo kuhusu mada fulani. Njia hii ilitoa nafasi kwa mwa Mtafiti na mtafitiwa kubadilishana mawazo.Hivyo ilisaidia mtafitiwa kutoa haraka taarifa au habari nyingi nzuri za kufaa.

### 3.5.2.4 Maktabani (Mbinu ya kimaktaba).

Maktaba ni eneo jingine ambalo mtafiti alikusanya data kutoka katika vitabu na makala mbalimbali.Utafiti huu ulifanyika katika maktaba ya Mkoa wa Mwanza, ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na ya Chuo Kikuu cha Dares salaam. Ewan na Calvet (2000), wanaeleza kuwa maktabani ni mahali maalum palipohifadhiwa nyaraka, vitabu, majarida na magazeti yenye taarifa mbalimbali kwa wasomaji na watafiti wa kada tofauti tofauti za taalam.

Maktaba hizi zilimsaidia mtafiti kupata mapitio mbalimbali kwani humo mtafiti alisoma vitabu, makala, tasnifu, magazeti na tafiti tangulizi zilizohusiana na mada ya utafiti wake na kufahamu kilichosemwa na watafiti wengine juu ya mada yake kisha aliweza kubaini pengo la utafiti alilolishughulikia.Data zilizopatikana ziliongezwa kwenye data zilizokusanywa maskanini ili kukamilisha madhumuni ya utafiti huu.

## 3.6. Mkabala wa uchambuzi wa data.

Data zilizokusanywa zilitolewa maelezo, zilichambuliwa na kufupishwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na wa kiidadi.  Kothari (1990), anaeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi ni njia ya kuchambua data katika muundo wa maelezo pasipo kufuata taratibu za kitakwimu.

Katika utafiti huu mkabala huu ulimwezesha mtafiti kuchambua data zilizokuwa katika maelezo kupitia njia ya mahojiano, majadiliano na  kwa kutumia hojaji lililoandaliwa na mtafiti.Aidha, jedwali lilitumika na hivyo data hizo  zilifupishwa kwa namna ambayo ni rahisi kuchambuliwa na kueleweka kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu.

### 3.7 Uchambuzi wa data.

Kothari (2008), anaeleza kuwa uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo zitasaidia kujibu maswali ya utafiti husika.

Data zilikusanywa kutoka vyanzo kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Mtafiti kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na wa kiidadi alichambua data hizo.

### 3.8 Vikwazo vya utafiti.

Katika utafiti huu kulikuwa na vikwazo ambavyo vilikuwa nje ya uwezo wa mtafiti. Hata hivyo mtafiti anatumaini kuwa vikwazo hivyo vitawasaidia watafiti wengine katika tafiti zijazo. Alikumbana na vikwazo vya:

**Lugha:** Data zingine alizikusanywa kutoka kwa wasiojua kuongea Kiswahili fasaha na sanifu. Hivyo ilimbidi amtafute mkalimani yaani mnyamwezi mzawa mmilisi wa lugha ya Kinyamwezi na Kiswahili ili awe akitafsiri maneno na sentensi za Kinyamwezi kwa Kiswahili na hali kadhalika sentensi na maneno ya Kiswahili ayatafsiri kwa Kinyamwezi. Ikawa hivyo. Hapa mtafiti alipata data toka kwa wazee wa kimila wamilisi wazawa wa lugha ya Kinyamwezi.Hawa walitoa maelezo kuhusu mila na desturi za Kinyamwezi na mapungufu yake kuhusiana na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili wa wanafunzi wanyamwezi.

**Usafiri:** Sehemu zingine mtafiti alipata taabu ya usafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine katika ukusanyaji wa data. Kutokana na sababu hiyo kuna wakati mtafiti alilazimika kutembea kwa miguu jambo ambalo lilimfanya mtafiti atumie muda mwingi na kuchoka sana kitendo ambacho kilimfanya mtafiti ashindwe

kufanya baadhi ya shughuli za kiutafiti pindi anaporudi toka kutafuta data. Baada ya kuonana na mtaalamu wa afya aliweza kupewa dawa za kutumia ili ziwe zikimwondolea maumivu.

## 3.9 Hitimisho.

Ushirikiano wa mtafiti na watafitiwa ulisaidia sana kukusanya taarifa zilizokusudiwa na hivyo kusaidia kubaini athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii imeonyesha taarifa zilizokusanywa wakati wa utafiti huu. Imehusisha uwasilishaji wa data na uchambuzi wa data. Taarifa hizi zilihusisha makundi matatu,Makundi hayo ni wanafunzi 23 wanyamwezi wa shule za sekondari wajifunzao lugha ya Kiswahili, walimu 08 wa shule za Msingi na Sekondari wataalamu wa lugha ya Kiswahili na Wazungumzaji 09 wamilisi wazawa wa lugha ya Kinyamwezi wakiwemo wazee mashuhuri wa mila na desturi.

## 4..2 Aina za fonimu za Kinyamwezi.

Habwe na Karanja (2004), wanaeleza kuwa, katika jedwali la IPA sauti za lugha zimeainishwa katika makundi mbalimbali kulingana na sifa zake bainifu. Kwa kutumia kigezo cha jinsi zinavyotamkwa, sauti za lugha zinagawanywa katika makundi mawili makuu: Konsonanti na vokali.

Kulingana na maelezo ya wataalam hao, fonimu za nusu irabu zimewekwa katika kundi la konsonanti na hivyo kuitwa konsonanti. Hivyo basi, tunaweza kusema kuwa lugha ya Kinyamwezi ina jumla ya konsonati 22 ( Zikiwemo nusu irabu 02 ).


Habwe na Karanja ( 2004), wanaeleza kuwa, kuna sifa nyingine za kimatumizi ambazo hutumika kufafanua aina za vokali. Sifa moja ni kama vile *urefu wa vokali* na *mkondohewa unaohusika.*

Vokali moja ikivutwa wakati wa kutamka neno, hivi kwamba isipovutwa neno litakuwa na maana tofauti, husemwa kuwa ni *vokali ndefu*.Vokali ndefu

huwakilishwa kiothografia kwa kurudia vokali hiyo. Kwa mfano maneno < kaka> na < kaakaa> hutofautishwa kimaana na vokali [α]ambayo ni fupi katika neno la kwanza na ndefu katika neno la pili. Vokali ndefu huonyeshwa kifonetiki kwa diakritiki [ **:** ] hivi kwamba maneno haya yatawakilishwa kifonetiki ifuatavyo: [ k α k α ] na [ ka:ka:].Maganga na Schadeberg (1992),wameeleza kuwa Kinyamwezi kina mfumo wa irabu saba . Hata hivyo mtafiti alipokuwa masikanini, aligundua kuwa Kinyamwezi kina irabu tano fupi.Kwa mfano katika maneno haya:

| **Irabu** | **Neno (Kinyamwezi)** | **Maana yake kwa Kiswahili** |
|---|---|---|
| / a / | β**a**ʧa / bhacha | Washa moto/gari/taa/mashine/ na kadhalika. |
| / ɛ / | [ β**ɛ**la ] bhela | Vunja |
| / i / | [ **i**golo ] igolo | Kesho |
| / ɔ / | [ s**o**la ] sola | Chukua |
| / u / | [ g**u**la gula | Nunua |


**Kielelezo Na.4.1 Fonimu za irabu fupi za Kinyamwezi.**




Massamba (2004:19 ), anaeleza kuwa irabu ndefu ni irabu ambayo huchukua wakati mrefu zaidi katika kutamkwa kwake. Akiwa huko huko masikanini, vilevile mtafiti aligundua kuwa Kinyamwezi pia kina irabu tano ndefu. Kwa mfano katika maneno haya:

| Irabu | Neno (Kinyamwezi) | Maana Yake Kwa Kiswahili. |
|---|---|---|
| / a: / | [ j**a**:ga ] jaaga | Nenda |
| / ε: / | [ εʃ **ε:** ma ] esheema | Pumua |
| / i: / | [ l**i**:ha] liiha | Refuka |
| / ɔ: **/** | [ yɔ:mba ] yoomba | Sema |
| / u:/ | [ t**u**:ŋga ] tuunga | Funga |

**KielelezoNa. 4.2 Fonimu za irabu ndefu za Kinyamwezi.**




**Kielelezo Na.4.3 Matriki ya irabu za Kinyamwezi.**

| **Irabu** | **/a /** | **/a: /** | **/ε /** | **/ε: /** | **/i /** | **/ i: /** | **/ ɔ /** | **/ ɔ:/** | **/u /** | **/ u: /** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Juu** | - | - | - | - | + | + | - | - | + | + |
| **Chini** | + | + | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Nyuma** | - | - | - | - | - | - | + | + | + | + |
| **Mbele** | - | - | + | + | + | + | - | - | - | - |
| **Mviringo** | - | - | - | - | - | - | + | + | + | + |
| **Urefu** | - | + | - | + | - | + | - | + | - | + |

**Kielelezo Na.4.4 JEDWALI LA KONSONANTI NA NUSU IRABU ZA KINYAMWEZI**

| **NAMNA YA KUTAM-KA** | **MAHALI PA KUTAMKIA** | | | | | | | | **HALI YA GLOTA** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Midomo | Midomo na Meno | Meno | Ufizi | Kaaka Gumu na Ufizi | Kaakaa Gumu | Kaakaa Laini | Koromeo | |
| Vizuiwa/ Vipasuo | | | | d | | | g | | Ghuna |
| | P | | | t | | | k | | Hafifu |
| Vizuiwa Kwamizwa | | | | | | / ɟ / | | | Ghuna |
| | | | | | | / ʧ / | | | Hafifu |
| Vikwa-Mizwa | β | v | | z | | | | h | Ghuna |
| | | f | | s | ʃ | | | | Hafifu |
| Nazali | m | ɱ | | n | | ɲ | ŋ | | Ghuna |
| Kitambaza | | | | l | | | | | Ghuna |
| Kimadende | | | | | | | | | Ghuna |
| Nusu Irabu | w | | | | | y | | | Ghuna |

**Tini wayo : Utafiti uliofanyikia maskanini wilayani Urambo**

Kama inavyoonekana katika jedwali hili hapo juu,Kinyamwezi hakina sauti /Θ/, /*ð*/ , / γ / ,/*x*/,/*r*/ na / *b* /. Aidha, Maganga na Schadeberg (1992), katika Dimendaal

(2011) wanaeleza kuwa, sauti / b / iliyomo katika lugha ya Kiswahili inawakilishwa na sauti /β/ iliyomo katika lugha ya Kinyamwezi. Kwa mfano katika neno la Kinyamwezi '*bhabha'* yaani yaani /βa:βa / badala badala ya '*baba'*.

**4.3 Athari ya Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili.**

Athari mbalimbali huweza kusababishwa na lugha mama wakati wa kujifunza lugha nyingine. Mtu anayejifunza lugha ambayo ni mpya kwake, hukumbana na vikwazo na changamoto nyingi zinazoweza kumtatiza na kumzuia wakati wa kujifunza lugha hiyo. Katika utafiti huu mtafiti alibaini athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza Kiswahili. Athari hizi ni za kimsamiati, kimatamshi na kimaana.

Chanzo cha data zifuatazo ni watafitiwa wanafunzi wa sekondari waliojibu hojaji iliyouliza wawapo nyumbani ni lugha ipi huwa wanaitumia zaidi katika mawasiliano.

**Kielelezo NA. 4.5 Jedwali la watafitiwa linaloonyesha idadi na majibu yao.**

| IDADI YA WANAFUNZI | KISWAHILI | KINYAMWEZI |
|---|---|---|
| 23 | 08 | 15 |

Kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapo juu, wanafunzi 08 ambao ni sawa na 35% walijibu kwamba,wawapo nyumbani hutumia zaidi lugha ya Kiswahili katika mawasiliano. Wanafunzi 15 ambao ni sawa na 65% walisema wawapo nyumbani hutumia zaidi lugha ya Kinyamwezi katika mawasiliano.

Walipoulizwa swali kuwa wawapo nje ya mazingira ya nyumbani na ya shuleni ni lugha ipi huwa wanaitumia zaidi katika mawasiliano, majibu yalikuwa ifuatavyo:

**Kielelezo Na .4.6 Jedwali la watafitiwa linaloonyesha idadi na majibu yao.**

| IDADI YA WANAFUNZI | KISWAHILI | KINYAMWEZI |
|---|---|---|
| 23 | 10 | 13 |

Kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapo juu,wanafunzi 10 ambao ni sawa na 43% walijibu kwamba,wawapo nyumbani hutumia zaidi lugha ya Kiswahili katika mawasiliano. Wanafunzi 13 ambao ni sawa na 57% walijibu kuwa wawapo nyumbani hutumia zaidi lugha ya Kinyamwezi katika mawasiliano .

Walipoulizwa kama ni kweli kuwa Kinyamwezi kimekiathiri Kiswahili kimsamiati majibu yalikuwa kama ifuatavyo:

**Kielelezo Na.4.7 Jedwali la watafitiwa linaloonyesha idadi na majibu yao.**

| IDADI YA WANAFUNZI | NDIYO | HAPANA |
|---|---|---|
| 23 | 19 | 4 |

Kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapo juu, wanafunzi 19 ambao ni sawa na 83% walijibu NDIYO. Wanafunzi 04 ambao ni sawa na 17% walijibu HAPANA . Waliojibu NDIYO walitaja maneno mbalimbali yaliyomo kwenye msamiati wa Kiswahili yaliyotokana na lugha ya Kinyamwezi. Miongoni mwa maneno hayo ni *mtemi, bunge na ikulu.*

Chanzo cha data zifuatazo ni watafitiwa walimu wa Msingi na wa Sekondari waliojibu hojaji iliyouliza kama kuna athari yoyote ya kimsamiati, kimatamshi na kimaana iliyosababishwa na lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza Kiswahili, walijibu kama ifuatavyo:

**Kielelezo Na.4.8 Jedwali la watafitiwa linaloonyesha idadi na majibu yao**.

| IDADI YA WALIMU | NDIYO | HAPANA |
|---|---|---|
| 08 | 08 | 00 |

Kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapo juu, walimu wote 08 ambao ni sawa na asilimia 100 walijibu NDIYO. Walimu hawa kwa kuwa walijibu NDIYO walitakiwa kutoa mifano ili kudhihirisha athari hiyo. Hivyo walitoa mifano ifuatayo:

**i. Athari ya kimsamiati.**

Baadhi ya wanyamwezi wajifunzao Kiswahili hufanya makosa ya kuingiza msamiati wa lugha ya Kinyamwezi katika lugha ya Kiswahili.

**Kielelezo Na.4.9 Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari za kimsamiati.**

| **Na.** | **KINYAMWEZI** | **KISWAHILI** |
|---|---|---|
| 1. | Lino lilisata . | Husema ‘*lino linasata’* badala ya kusema ‘jino linauma’. |
| 2**.** | Nokokunkuguma | Husema ‘*nitakukunkuguma’* badala ya kusema ‘ *nitakupiga*’. |
| 3. | Mayo alesunta | Husema ‘mama *anasunta*’ badala ya kusema ‘*mama anachechemea*’. |
| 4. | Kapaya wagulaga shenene | Husema *‘Kapaya amenunua shenene’* badala ya kusema *‘Kapaya amenunua senene’* |
| 5. | Mayo alesunta. | Husema ‘mama *anasunta*’ badala ya kusema ‘*mama anachechemea*’. |

Data hii inaonyesha jinsi Mwanafunzi mnyamwezi anayejifunza Kiswahili anavyotumia msamiati wa Kinyamwezi azungumzapo sentensi za Kiswahili.

### ii. Athari za kimatamshi.

Baadhi ya wanyamwezi wajifunzao Kiswahili hufanya makosa ya kubadili matamshi sahihi ya sauti wakati wanapotamka neno na badala yake kutumia matamshi yasiyo sahihi.Makosa hayo si tu hufanya neno linalotamkwa kutokuwa sahihi, bali pia huweza kupoteza maana ya neno lenyewe.

Yule (2010), anasema kuwa, matamshi ni utamkaji wa sauti za binadamu kwa kuzingatia muktadha wa mazungumzo.Nkwera (1979), anaeleza kuwa, muhimili wa mawasiliano mazuri ni utoaji wa matamshi yanayoeleweka kwa msikilizaji.

Baadhi ya wanyamwezi wajifunzao Kiswahili hufanya makosa ya kubadili matamshi sahihi ya sauti wakati wanapotamka neno na badala yake kutumia matamshi yasiyo sahihi.Makosa hayo si tu hufanya neno linalotamkwa kutokuwa sahihi, bali pia huweza kupoteza maana ya neno lenyewe.

#### a) A**thari katika matumizi ya /r/**

Fonimu hiyo ni kimadende na ni sauti ya ufizi. Hutamkwa wakati hewa ikisukumwa kwa nguvu kiasi cha kusababisha mtetemeko kwenye ulimi na kugotagota kwenye ufizi. Huhusisha bapa la ulimi kama ala sogezi na mwinuko wa ufizi ulio nyuma ya meno ya juu ukiwa ndio alatuli.

Sauti / r / hupotoshwa na kuwa / l / yaani silabi **ra, re, ri, ro, ru** hupotoshwa na kuwa ***la***, ***le, li, lo, lu***.

**Kielelezo na.4.10 Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari katika matumizi ya /r/**

| ***Na.*** | ***Athari ya umbo katika Kiswahili*** | ***Umbo sahihi*** |
|---|---|---|
| *1.* | *lusha* | *rusha* |
| *2.* | *malazi* | *maradhi* |
| *3.* | *Tabola* | *Tabora* |
| *4.* | *fahali* | *fahari* |

Sauti /l/ na /r/ zote ni vilainisho na ni sauti za ufizi.Wakati zitamkwapo ulimi ambao ni ala sogezi hugusana na ufizi ambao ni ala tuli.

b) **Athari katika matumizi ya / γ /**

Fonimu hiyo ni kikwaruzo na ni sauti ya kaakaa laini (kaakaa la nyuma). Ni sauti ya nyuma kwani utamkaji wa sauti hii huambatana na sehemu ya nyuma ya ulimi, ambao ni alasogezi, kugusa kaakaa laini, ambalo ni ala sogezi pia. Hutamkwa wakati alasauti zinapokaribiana na kupunguza upenyo wa bomba la sauti kiasi cha kufanya hewa ipite kwa shida kiasi cha kusababisha mkwaruzo.

Sauti / γ / hupotoshwa na kuwa / g / yaani silabi **gha, ghe, ghi, gho, ghu** hupotoshwa na kuwa ***ga***, ***ge, gi, go, gu***.

**Kielelezo na.4.11 Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari katika matumizi ya /γ/**

| ***Na.*** | ***Athari ya umbo katika Kiswahili*** | ***Umbo sahihi*** |
|---|---|---|
| *1.* | *luga* | *lugha* |
| *2.* | *golofa* | *Ghorofa* |
| *3.* | *galama* | *Gharama* |
| *4.* | *agalabu* | *Aghalabu* |

Sauti /g / na / γ / zote ni za kaakaa laini.Utamkwaji wake huandamana na sehemu ya nyuma ya ulimi, ambao ni ala sogezi kugusa kaakaa laini,ambalo ni alatuli.

*c)* **Athari katika matumizi ya** / Ɵ /

Fonimu hii ni kikwamizi na ni sauti ya meno. Hutamkwa wakati ncha ya ulimi ikiweka katikati ya meno ya juu na ya chini.Katika utamkaji wa sauti hii, badala ya mkondohewa kubanwa kabisa, huachiwa kupita lakini kwa kugusanisha alasogezi na alatuli kiasi kwamba sauti hutoka kwa kukwamakwama. Hii ni sauti ambayo katika utamkaji wake badala ya mkondohewa kubanwa kabisa,huachiwa kwa kukwamakwama**.**

Sauti / Ɵ / hupotoshwa na kuwa / s / yaani silabi **tha, the, thi, tho, thu** hupotoshwa na kuwa ***sa***, ***se, si, so, su***.

**Kielelezo na.4.12 Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari katika matumizi ya /Ɵ/**

| *Na.* | **Athari ya Umbo Katika Kiswahili** | **Umbo Sahihi** |
|---|---|---|
| *1.* | *semanini* | *themanini* |
| *2.* | *sawabu* | *thawabu* |
| *3.* | *tasmini* | *tasthmini* |
| *4.* | *samani* | *Thamani* |

Sauti /s/ na / Ɵ / zote ni vikwaruzo. Hutamkwa wakati ala za sauti zinapokaribiana na kupunguza upenyo wa bomba la sauti kiasi cha kufanya hewa ipite kwa shida na hivyo kusababisha mkwaruzo.

*d)* **Athari katika matumizi ya** ***/ ð, /***

Fonimu hii ni kikwamizi na ni sauti ya meno. Ni sauti ambayo katika utamkaji wake badala ya mkondohewa kubanwa kabisa, huachiwa kwa kukwamakwama. Hutamkwa wakati ncha ya ulimi ikiweka katikati ya meno ya juu na ya chini.Katika utamkaji wa sauti hii, badala ya mkondohewa kubanwa kabisa, huachiwa kupita lakini kwa kugusanisha alasogezi na alatuli kiasi kwamba sauti hutoka kwa kukwamakwama**..**

Sauti / *ð,* / hupotoshwa na kuwa / z / yaani silabi **dha, dhe, dhi, dho, dhu** hupotoshwa na kuwa ***za***, ***ze, zi, zo, zu***.

**Kielelezo na.4.13 Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari katika matumizi ya /ð/**

| *Na.* | **Athari ya Umbo Katika Kiswahili** | **Umbo Sahihi** |
|---|---|---|
| *1.* | *Zahabu* | *dhahabu* |
| *2.* | *Zambi* | *dhambi* |
| *3.* | *Zoluba* | *dhoruba* |
| *4.* | *Zalimu* | *dhalimu* |

Sauti /z/ na */ ð, /* zote ni vikwaruzo.Hutamka wakati ala za sauti zinapokaribiana na kupunguza upenyo wa bomba la sauti kiasi cha kufanya hewa ipite kwa shida na hivyo kusababisha mkwaruzo.

e) **Athari katika matumizi ya */ b /***

Fonimu hii ni kizuiwa (kipasuo) na ni sauti ya mdomo. Wakati wa kuitamka mdomo wa chini huelekeana na mdomo wa juu.Katika utamkaji wa sauti hii, mkondohewa kutoka mapafuni husukumwa nje kwa nguvu na kuzuiliwa kabisa mahali pa kuitamkia na kisha kuachiliwa ghafla.

Sauti / b / hupotoshwa na kuwa / β / yaani silabi **ba, be, bi, bo, ba** hupotoshwa na kuwa **bha, bhe, bhi, bho, bhu** .

**Kielelezo na.4.14 Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari katika matumizi ya /*b* /**

| ***Na.*** | **Athari ya Umbo Katika Kiswahili** | **Umbo Sahihi** |
|---|---|---|
| *1.* | *baba* | *bhabha* |
| *2.* | *bahati* | *bhahati* |
| *3.* | *mabango* | *mabhango* |
| *4.* | *bonge* | *bhonge* |

Sauti / b / na /β/ zote ni sauti za midomo ingawa Sauti / b / ni kizuiwa,hutamkwa wakati mkondohewa unapofungiwa kabisa katika sehemu yoyote ya bomba la sauti na kisha kuruhusiwa upite ghafla. Na sauti /β/ ni kikwamizwa,hutamkwa wakati ala sauti zinapokaribiana na kupunguza upenyo wa bomba la sauti kiasi cha kufanya hewa ipite kwa shida na hivyo kusababisha mkwaruzo.

f). **Uchopekaji wa sauti au silabi katika neno.**

Massamba (2004),anaeleza kuwa, uchopekaji ni uingizaji wa irabu, kiyeyusho au konsonanti katika neno.

Baadhi ya wazungumzaji wa Kinyamwezi huchopeka silabi mojawapo miongoni mwa *ga*,*ge*,*gi*,*go* na *gu* wakati wa ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili wazungumzapo sentensi za Kiswahili. Kwa hali hiyo huzungumza Kiswahili potofu badala ya Kiswahili Sanifu.

**Kielelezo na.4.15 Jedwali linaloonyesha mifano ya Uchopekaji wa silabi katika neno.**

| *Na.* | **Athari ya Umbo Katika Kiswahili** | **Umbo Sahihi** |
|---|---|---|
| *1.* | *Wa**ga** naenda shuleni* | *Huwa ninakwenda shuleni.* |
| *2.* | *Ninaenda**ga** kanisani* | *Huwa ninakwenda kanisani.* |
| *3.* | *Salome haimba**gi** vizuri* | *Salome huwa haimbi vizuri.* |
| *4.* | *Juma anacheza**ga** mpira* | *Juma huwa anacheza mpira.* |

Vilevile huchopeka silabi ***ga*** badala ya silabi ***ya*** au ***ka*** katika sentensi.Kwa mfano:

**Kielelezo na.4.16 Jedwali linaloonyesha mifano ya Uchopekaji wa silabi katika neno.**

| **Na.** | **Kiswahili potofu** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|---|
| 1. | *Mahindi **ga**menunuliwa* | *Mahindi **ya**menunuliwa.* |
| 2. | *Maji **ga**meisha* | *Maji **ya**meisha.* |
| 3. | *Pi**ga** Chakula* | *Pi**ka** chakula.* |

Hali kadhalika kutokana na kuathiriwa huko, huchopeka sauti katika maneno waongeapo sentensi za Kiswahili.Kwa mfano:

**Kielelezo na.4.17 Jedwali linaloonyesha mifano ya Uchopekaji wa sauti katika neno.**

| Na. | Kinyamwezi | Kiswahili |
|---|---|---|
| 1. | Kapaya wagulaga s**h**enene | Husema *'Kapaya amenunua s**h**enene'* badala ya kusema *'Kapaya amenunua senene.* |
| 2. | Mayu wajaga kukagula **n**samaki . | Husema *'Mama amekwenda kununua **n**samaki* badala ya kusema *'Mama amekwenda kununua samaki'* |

g). **Udondoshaji wa sauti.**

Massamba (2004), anaeleza kuwa udondoshaji sauti ni uondoaji, ama kwa makusudi au kwa bahati mbaya, wa sauti moja au mbili katika neno. Kwa kawaida udondoshaji wa sauti huwa ni wa namna tatu:Udondoshaji sauti awali yaani uondoaji wa sauti mwanzoni mwa neno, udondoshaji sauti kati yaani uondoaji wa sauti katikati ya neno na udondoshaji sauti tamati yaani uondoaji wa sauti mwishoni mwa neno.

Baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kinyamwezi huathiriwa na lugha yao kiasi kwamba wazungumzapo lugha ya Kiswahili hudondosha baadhi ya sauti. Kwa mfano:

| **Kinyamwezi** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Numba iyo yabomokaga. | Husema 'numba *hiyo imebomoka'* badala ya kusema *'n**y**umba hiyo imebomoka'*. |

Tukiangalia mfano huo hapo juu tunaona kuwa sauti / ***j*** / ya neno nyumba imedondoshwa, neno hilo likapotoshwa na kuwa *'numba'*.

Athari zingine za kimatamshi hujitokeza wakati wanafunzi hao wazungumzapo sentensi za Kiswahili kwani huzungumza Kiswahili potofu badala ya Kiswahili Sanifu, kwa mfano :

| **Kiswahili potofu** | **Kiswahili sanifu** |
|---|---|
| ***Sibhitali*** *hizo zinavutia* | *Hospitali hizo zinavutia.* |

**iii).Athari za kimaana.**

Mtafiti aliweza kubaini kuwa baadhi ya wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kinyamwezi wajifunzao lugha ya Kiswahili, wazungumzapo lugha ya Kiswahili hutafsiri maneno au sentensi zilizoko katika lugha yao na kuitumia katika lugha ya Kiswahili.Wakati mwingine tafsiri hiyo huwa ni sisisi.Hali hii husababisha athari za kimaana katika lugha ya Kiswahili.Hebu tuone mifano ifuatayo:

Mfano wa kwanza:

**Kielelezo na.4.18 Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari za kimaana.**

| **Na.** | **Kinyamwezi** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| 1. | Namsanga | Nimemkuta |
| 2. | Kuduhu | Hayupo |
| 3. | Namsanga kuduhu | Nimemkuta hayupo |

Hapa inaonyesha kuwa mzungumzaji huyo wa Kinyamwezi husema kuwa, ‘*Namsanga kuduhu’* akimaanisha ‘*Sijamkuta’* lakini azungumzapo Kiswahili akimaanisha ‘*Sijamkuta’* husema , ‘*Nimemkuta hayupo’*.Hili pia ni kosa la kimantiki.

Mantiki ni utaratibu mzuri wa kufikiri.Makosa ya kimantiki ni yale yanayoonyesha kukosekana kwa utaratibu wa fikira.

Mfano wa pili:

| Kinyamwezi | Kiswahili |
|---|---|
| Igolo | Kesho |
| Igolo | Jana |

Hapa tunaona kuwa, kwa Kinyamwezi neno ‘igolo’ huwa na maana mbili, maana ya kwanza ni *‘kesho’* na maana ya pili ni *‘jana’*.Hivyo baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kinyamwezi hudhani kuwa hata katika lugha ya Kiswahili huwa vivyo hivyo.Kwa mfano wao husema *‘Nitakuja jana’* wakimaanisha kuwa, *‘Nitakuja kesho’*.Hali kadhalika huweza kusema,’Nilikuja kesho’ wakimaanisha *‘Nilikuja jana’*.Fasili za maneno *‘kesho’ na ‘jana’* huwachanganya na kiasi cha kuwafanya wazitumia kinyume wazungumzapo Kiswahili.

Mfano wa tatu:

| Kinyamwezi | Kiswahili |
|---|---|
| kabhula | badala |

Hapa tunaona kuwa mnyamwezi huyo anayejifunza Kiswahili hulitumia neno *‘kabla’* akimaanisha *‘badala’*.Kwa mfano asemapo *‘Kabhula ya kuzuga wali obhebhe ulizuga bhugali!’* akimaanisha, *‘Badala ya kupika wali wewe unapika ugali!*

Katika lugha ya Kinyamwezi, ni desturi ya Wanyamwezi kutumia wingi badala ya umoja katika baadhi ya sentensi ili kudhihirisha heshima kwa wanayezungumza naye. Kwa mfano wasemapo:

**Kielelezo na.4.19 Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari za kimaana.**

| Na. | Kinyamwezi | Maana yake kwa Kiswahili | Kilichomaanishwa na msemaji |
|---|---|---|---|
| 1. | *Bhabha, solagi chakulya.* | *Baba, chukueni chakula.* | *Kilichomaanishwa na msemaji.* |
| 2. | *Tupagi minzi ganaya* | *Tupeni maji haya.* | *Nipe maji haya.* |

Kama tunavyoona hapo juu, baadhi ya Wanyamwezi huihamishia desturi hiyo katika Kiswahili.Kwa hiyo azungumzapo Kiswahili hujikuta akitumia wingi akimaanisha umoja katika sentensi ili kuonyesha heshima kwa anayezungumza naye.

Idarus (2005),ametaja athari zinazojitokeza katika lugha ya Kiswahili baada ya mtu kuathiriwa na mambo kadhaa kuwa ni pamoja na kuongeza vitamkwa ama sauti pasipohitajika,msamiati wa lugha,makosa ya muundo wa sentensi na makosa katika matamshi.

Ingawa makosa hayo ya kimsamiati, kimatamshi na kimaana yamezoeleka na kuonekana kuwa ya kawaida miongoni mwa watumiaji wa Kiswahili na kwamba kinachozungumzwa hueleweka kwa wasikilizaji, hutia doa katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, wakati mwingine huweza kuathiri mawasiliano pale neno lililokosewa linapochukua maana nyingine kwa mfano mzungumzaji mnyamwezi anapotamka neno ***samani*** badala ya ***thamani,*** ***fahali*** badala ya ***fahari*** ***malazi*** badala ya ***maradhi,*** na ***shindano*** badala ya ***sindano.***au anapotumia neno ***kabla*** kwa kumaanisha ***badala*** au neno ***kesho*** akimaanisha ***jana***. ,Huenda hawafanyi makosa

haya kwa makusudi na pengine hawatambui kuwa wanatamka ama kuzungumza kimakosa.

Walimu hawa walipoulizwa ni sababu zipi huchangia kuwaathiri wanafunzi wanyamwezi katika kujifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili miongoni mwao walijibu ifuatavyo:

Sababu kuu ya athari za kimatamshi ni ndimi za wahusika kuathiriwa na lugha mama ,ukosekana kwa sauti / r /,/ γ /,/ ϴ / na / ð / na / b / katika lugha ya Kinyamwezi na kukosekana kwa baadhi ya msamiati wa lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kinyamwezi. Kutokana na wanafunzi hao kutokuwa na msamiati wa kutosha wa lugha ya Kiswahili ambapo uhaba huu huwafanya wahalalishe msamiati wa Kinyamwezi kuwa wa Kiswahili na hivyo kutumia maneno yasiyosanifiwa .Kwa mfano:

**Kielelezo na.4.20 Jedwali linaloonyesha mifano ya Athari za kimaana.**

| Na. | **Msamiati wa Kinyamwezi** | **Maana yake kwa Kiswahili** |
|---|---|---|
| 1. | *Matole* | *Nyanya mshumaa* |
| 2. | *Kusunda* | *Kutoa vyombo viliyotumika kuwekea na kulia Chakula.* |
| 3. | *Matoborwa* | *Viazi vilivyopikwa na kukaushwa* |
| 4. | *Nhwili* | *Tui la karanga* |
| 5. | *Mgubi* | *Kibarua* |

Uhaba wa walimu wa lugha ya Kiswahili ni kisababisho pia..Aidha, Baadhi ya walimu wawafundishao wajifunzao lugha ya Kiswahili huwa hawana umilisi wa lugha ya Kiswahili.Ujuzi mdogo wa lugha ya kufundishia huwa na athari hasi kwa ufundishaji na ujifunzaji. Mwanafunzi hujifunza lugha kwa kusikia namna azungumzavyo mwalimu wake. Kwa mfano,mwanafunzi anaposikia matamshi mabaya kutoka kwa mwalimu wake,mara nyingi na yeye hufanya makosa hayo bila kujua. Hii ni kwa sababu mwalimu ni mzungungumzaji wa lugha ya kwanza.

Vilevile ufundishaji mbaya wa walimu wengi wa lugha ya Kiswahili huchangia. Mkakati wa ufundishaji mbaya wa lugha ya pili kutokana na welewa mbaya wa mwalimu ni kikwazo kwani walimu wengi wafundishao Kiswahili huwa hawachagui mbinu bora za kufundishia na kuzitumia ipasavyo wafundishapo.Vilevile huwa hawatayarishi zana bora za kufundishia na kujifunzia na hawazitumii itakiwavyo katika harakati za ufundishaji na ujifunzaji. Kutokana na walimu hao kutogundua kuwa wao ni chanzo cha tatizo, wakati mwiingine wao huweza kudhani kuwa wanafunzi kutokuwa wepesi wa kuelewa kuzungumza ipasavyo lugha ya Kiswahili husababishwa na wanafunzi hao kuwa na tabia ya uvivu, uwezo mdogo wa kiakili au kutotaka kutoa ushirikiano. Mtazamo wa aina hii unaweza kuwa kikwazo kikubwa kwa wanafunzi na kuwajengea woga wa kujifunza lugha ngeni.Alidou na Brock-utne, (2006:87), wanaeleza kuwa ili kuogopa kuaibika kwa wenzao, baadhi ya wanafunzi huacha kujitolea kujibu maswali.

Zaidi ya hayo,wanafunzi kutopata muda wa kutosha kujifunza na kuzungumza Kiswahili wawapo nje ya mazingira ya shule ni changamoto .Pia ukosefu wa sheria zenye tija ya kukataza kuongea Kinyamwezi shuleni huchangia. Kwenye shule nyingine hata kama sheria hiyo ipo, aidha hakuna ufuatiliaji ama haitiliwi mkazo.

Kingine ni wazazi na watoto wao kutoona umuhimu wa lugha ya Kiswahili na somo la Kiswahili. Hali hii huwafanya wapuuzie kujifunza lugha hii na somo la Kiswahili. Kutokana na hali hii wazazi huwa hawaupi kipaumbele ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na hivyo hawawahamasishi kwa kiasi cha kutosha watoto wao kujifunza na kuzungumza Kiswahili.Aidha,watoto hao hawaweki jitihada katika kujifunza Kiswahili.

Kwa upande mwingine,unasaba na mwingiliano baina ya lugha hizi mbili huchangia pia. Kwa mfano unavyojidhihirisha katika vipengele vya :

a. **Mofolojia:**Katika kutenganisha viambishi hufuata kanuni moja kwamba mahali panapokaa kiambishi kwa mfano cha njeo ndipo pia hukaa kwa upande wa lugha ya Kinyamwezi.Kwa mfano:

| **Kiswahili** | **Kinyamwezi** |
|---|---|
| Ni-***na***-imb-a | Na-***li*** –imb-a |
| Tu-***li***-imb-a | Tu-***ki***-imb-a |

**b. Msamiati:** Asilimia 60 ya maneno yote yanayoweza kutamkika na kuandikwa katika lugha ya Kiswahili asili yake ni lugha za Kibantu kikiwemo Kinyamwezi. Kwa mfano maneno *Mtemi* na *Ikulu*.

**c.Tungo:** Miundo ya tungo (sentensi za Kiswahili) zinafanana sana na miundo ya tungo za maneno ya Kibantu. Kwa mfano sentensi za Kiswahili na za Kinyamwezi zina kiima na kiarifu.

| **Kiswahili** | **Kinyamwezi** |
|---|---|
| *Kapuya anakwenda Tabora* | *Kapuya alija Nhobhola.* |
| *Ali anakula maharage* | *Ali alilya mahalage.* |

**d. Ngeli za Majina.** Wataalamu wanakubaliana kuhusu ngeli za majina kuwa kwa mujibu wa maumbo ya nomino (umoja na wingi wa majina) pamoja na

upatanisho wa kisarufi katika sentensi za Kiswahili hufanana na wa kibantu, Kinyamwezi kikiwemo.Kwa mfano:

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| **Kiswahili** | *Nyumba yangu imeungua* | *Nyumba zetu zimeungua* |
| | *Kiti changu kimevunjika* | *Viti vyetu vimevunjika.* |
| **Kinyamwezi** | *Numba yane yapyaga* | *Numba ziswe zyapyaga.* |
| | *Isumbe lyane lyabheleka* | *Masumbe gane gabheleka.* |

Vipengele vingine vinavyoangaliwa kuthibitisha unasaba uliopo kati ya Kiswahili na Kinyamwezi ni pamoja na vya kisintakisia na mizizi ya msamiati wa msingi kwani vina mfanano mkubwa na ule wa kibantu kikiwemo Kinyamwezi**.**

Walipoulizwa mbinu gani zitumike ili kuwasaidia wanafunzi wanyamwezi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili, miongoni mwao walitaja na kufafanua kama ifuatavyo:

Wanafunzi wapewe na kufanya mazoezi ya lugha mengi ya kutosha na kuyafanya yakiwemo yale ya kutunga sentensi zenye msamiati, miundo, uandikaji wa insha na kutamka maneno na sentensi zenye vitatiza ndimi. Mashindano ya midahalo ihusuyo lugha ya Kiswahili yafanyike shuleni, wanafunzi washindanishwe, washindi wapewe motisha.

Vilevile Jamii,koo,wazazi na wanafunzi, waelimishwe kuhusu faida za lugha ya Kiswahili na matumizi yake kwa mtu binafsi,familia,koo,jamii taifa na kimataifa (uhamasishaji ufanyike kwao ili kuwaibulia ufahamu huo).Waelimishwe juu ya umuhimu wa somo la Kiswahili. Aidha, Serikali iwape motisha wanafunzi wanaofaulu somo la Kiswahili kama ilivyo kwa wanaofaulu somo la Sayansi.

Si hivyo tu,bali pia wanafunzi wapewe muda wa kutosha kujifunza Kiswahili shuleni na nje ya mazingira ya shule kama vile nyumbani na maeneo mengine.Wapewe na kufanya mazoezi ya kutosha ya kukisoma na kukiongea Kiswahili.Ni muhimu kuweka majarida, magazeti na vitabu mbalimbali vya hadithi vya kutosha shuleni vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili ili wanafunzi wawe wakivisoma na hivyo kujifunza Kiswahili kwa njia ya usomaji. Hii itawawezesha kuwa na msamiati mwingi, kutamka maneno vizuri na hatimaye kuwajengea moyo wa kujiamini wazungumzapo lugha ya Kiswahili. Msau (2001), ameeleza kuwa, mijadala, michezo na usomaji wa magazeti huendeleza mawasiliano na kukuza lugha kwa mzungumzaji.

Ni jambo la busara kuchukua hatua dhidi ya upungufu wa walimu wenye ujuzi wa kutosha wa kufundisha somo la Kiswahili shuleni na vyuoni ili kuhakikisha kuwa shule na vyuo hivyo vinakuwa na walimu hao wa kutosha.Aidha,walimu wafundishao Kiswahili kama lugha au kama somo wateue na kutumia ipasavyo mbinu za kufundishia na kuhakikisha wanatayarisha na kutumia vema zana za kufundishia na kujifunzia wakati wa tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji.Walimu wafundishao vizuri lugha na somo la Kiswahili wapongezwe na kupewa motisha pia.Motisha hiyo pia iwe yenye kuleta faida kwenye ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili.

Chanzo kingine cha data kilitoka kwa wazungumzaji wazawa wamilisi wa lugha ya Kinyamwezi. Hawa walipoulizwa kama wao ni wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kinyamwezi majibu yalikuwa kama ifuatavyo:

**Kielelezo Na.4.21 Jedwali la watafitiwa linaloonyesha idadi na majibu yao.**

| IDADI YA WAMILISI WAZAWA WA LUGHA YA KINYAMWEZI | NDIYO | HAPANA |
|---|---|---|
| 09 | 09 | 00 |

Kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapo juu, wazungumzaji wamilisi wazawa wa lugha ya Kinyamwezi wote 09 ambao ni sawa na 100 walijibu NDIYO.

Walipoulizwa ni lugha gani inayotumika zaidi katika mawasiliano na wanafamilia yao wawapo nyumbani, majibu yalikuwa ifuatavyo:

**Kielelezo Na.4.22 Jedwali la watafitiwa linaloonyesha idadi na majibu yao.**

| IDADI YA WAMILISI WAZAWA WA LUGHA YA KINYAMWEZI | KISWAHILI | KINYAMWEZI |
|---|---|---|
| 09 | 01 | 08 |

Kama inavyoonyesha hapo juu, wamilisi wazawa wa lugha ya Kinyamwezi 08 sawa na asilimia 89 walijibu KINYAMWEZI na 01 sawa na asilimia 11 alijibu KISWAHILI.

Walipoulizwa kama wanafamilia Wanyamwezi wanaojifunza Kiswahili huongea Kiswahili sanifu walijibu kama ifuatavyo:

**Kielelezo na.4.23 Jedwali la watafitiwa iinaloonyesha Idadi na majibu yao.**

| IDADI YA WAMILISI WAZAWA WA LUGHA YA KINYAMWEZI | HAPANA | NDIYO |
|---|---|---|
| 09 | 09 | 00 |

Kama inavyoonyesha hapo juu, wamilisi wazawa wote 09 sawa na asilimia 100 walijibu HAPANA.

Kwa kuwa walijibu HAPANA, walitakiwa kueleza sababu zinazochangia athari za lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza Kiswahili, kwa ujumla walieleza ifuatavyo:

Mila na desturi za Kinyamwezi huwa haziupi kipaumbele ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.Mazingira wanayoishi wazazi hutumia lugha mama zaidi.Data zimeonyesha kuwa wanafunzi walio wengi warudipo toka shule yaani wawapo nyumbani, huwa hawatumii tena lugha ya Kiswahili katika mawasiliano.

Kulingana na mila na desturi hizo,salaam na mazungumzo mengine hutakiwa kufanyika kwa lugha ya Kinyamwezi. Hata salaam ya heshima kwa wakubwa itolewayo kwa Kiswahili yaani *'Shikamoo'*, kwa wanyamwezi huonekana kuwa haina uzito kama ya Kinyamwezi.Kinyamwezi huwa ni lugha ya familia, koo na jamii.Hivyo Katika familia na koo nyingi za Kinyamwezi, hakuna anayeruhusiwa kutumia Kiswahili katika kuwasiliana wawapo nyumbani.Anayekiuka mwiko huo huweza kuchukuliwa hatua kama adhabu na hata pengine mkosefu huyo huweza kutengwa na familia au ukoo wake.

Wanyamwezi hupenda kuzungumza lugha yao. Kwa hiyo katika hili hupenda sana kuienzi.Katika kufanya hivi hujikuta wamewaambukiza watoto wao tabia hii.Jambo hili huwanyima watoto hao muda wa kutosha kujifunza na kuzungumza Kiswahili katika mazingira wanayoishi.Licha ya hayo, pamoja na wanafunzi kufundishwa Kiswahili,hukosa muda wa kukifanyia mazoezi kwa kukizungumza kwa hiyo wakati mwingine huweza kusahau msamiati,matamshi au maana na matumizi ya baadhi ya maneno.

Rocha (2011), anasema kuwa wabantu wengi wameathiriwa na lugha mama,hii ni kutokana na matumizi ya lugha mama. Idarus (2005),ametaja athari zinazojitokeza katika lugha ya Kiswahili baada ya mtu kuathiriwa na mambo kadhaa kuwa ni pamoja na kuongeza vitamkwa ama sauti pasipohitajika,msamiati wa lugha,makosa ya muundo wa sentensi na makosa katika matamshi.

Paul (2001), anaeleza kuwa muktadha hupewa nafasi muhimu katika ufundishaji,hivyo mwanafunzi anapojifunza lugha fulani,mazingira ni muhimu kuangaliwa. Idarus (ameishatajwa.), katika Taasisisi ya Uchunguzi wa Kiswahili anaendelea kueleza kuwa maeneo yanayochangia ni pamoja na mazingira.

Dixon (1992), anaeleza kuwa uhusiano wa lugha ni baina ya jamii husika au wazazi, watoto na ndugu katika ukoo.Lugha inaweza kukua kuanguka au kuathiriwa kutokanana kuwepo na matumizi ya lugha nyingine katika jamii hiyo.

**4.4.Hitimisho.**

Sura hii imewasilishwa na kuchambua data zilizokusanywa katika utafiti huu ambazo zimepatikana kwa kutumia mbinu ya hojaji,mahojiano,majadiliano na

maktabani.Uwasilishaji wa uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti huu na umeongozwa na mkabala wa kimaelezo na wa kiidadi.Aidha,nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia iliyotumika katika utafiti huu imesaidia kuchanganua data za utafiti na kuweka wazi majibu ya maswali ya utafiti huu.

# SURA YA TANO

## 5.1 Utangulizi.

Sura hii ilihitimisha utafiti huu. Mambo yaliyoonyeshwa ni Utangulizi, Muhtasari wa utafiti huu, mchango wautafiti , mapendekezo na hitimisho kuhusiana na utafiti huu.

## 5.2 Muhtasari wa utafiti.

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza athari za Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Kiswahili. Aidha, utafiti huu umedhihirisha athari hizo katika viwango vya msamiati matamshi na maana.Kwa upande wa msamiati imebainika kuwa baadhi ya wanyamwezi wajifunzao Kiswahili hufanya makosa ya kuingiza msamiati wa lugha ya Kinyamwezi katika lugha ya Kiswahili.

Kwa upande wa matamshi imebainika kuwa Baadhi ya wanyamwezi wajifunzao Kiswahili hufanya makosa ya kubadili matamshi sahihi ya sauti wakati wanapotamka neno na badala yake kutumia matamshi yasiyo sahihi.Makosa hayo si tu hufanya neno linalotamkwa kutokuwa sahihi, bali pia huweza kupoteza maana ya neno lenyewe. Baadhi ya wazungumzaji wa Kinyamwezi huchopeka silabi mojawapo miongoni mwa *ga,ge,gi,go* na *gu* na pia hudondosha baadhi ya sauti wakati wa ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili wazungumzapo sentensi za Kiswahili.

Kwa upande wa maana imebainika kuwa baadhi ya wazungumzaji wazawa wa lugha ya Kinyamwezi wajifunzao lugha ya Kiswahili, wazungumzapo lugha ya Kiswahili hutafsiri maneno au sentensi zilizoko katika lugha yao na kuzitumia katika lugha ya Kiswahili

Matokeo ya utafiti yamebainisha sababu za lugha ya Kiswahili kuathiriwa na Kinyamwezi katika viwango tajwa hapo juu vya kiisimu yakiwa ni pamoja na ndimi za wahusika kuathiriwa na lugha mama,kukosekana kwa sauti / r /,/ γ /,/ Ɵ / na / ð / na / b / katika lugha ya Kinyamwezi, kukosekana kwa baadhi ya msamiati wa lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kinyamwezi, Ufundishaji mbaya wa walimu wa lugha ya Kiswahili, Wanafunzi kutopata muda wa kutosha kujifunza na kuzungumza Kiswahili wawapo nje ya mazingira ya shule na Wazazi na watoto wao kutoona umuhimu wa lugha ya Kiswahili na somo la Kiswahili.

Utafiti huu umebainisha mbinu za kutumia ili kuwasaidia wanafunzi wanyamwezi wanaojifunza Kiswahii kama lugha ya pili zikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapewa muda wa kutosha wa kufanya mazoezi ya lugha mengi ya kutosha.Walimu waeleweshwe na kuhamasishwa kuzitumia mbinu faafu katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.Aidha, Vilevile Jamii,koo,wazazi na wanafunzi, waelimishwe kuhusu faida za lugha ya Kiswahili na matumizi yake kwa mtu binafsi,familia,koo,jamii taifa na kimataifa (uhamasishaji ufanyike kwao ili kuwaibulia ufahamu huo.

**5.3 Mchango wa utafiti**

Utafiti huu utaibua ari za watafiti wengine na hasa katika kutafiti athari za lugha mama za Kibantu katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Tukirejelea katika kazi ya Onyango (1997), Ndun'gu ( 1999), na Mutugu (2001) tutaona kuwa watumiaji wengi wa Kiswahili kama lugha ya pili hukumbwa na matatizo katika matumizi yake ya lugha ya pili.Wazungumzaji wa lugha mbalimbali za asili Kinyamwezi kikiwemo ambao huzungumza lugha ya Kiswahili sanifu kama lugha yao ya pili nao huathiriwa na sauti za lugha yao katika katika vipengele vyote vya kiisimu yaani

Kisemantikia, Kifonolojia, Kimofolojia na Kisintaksia wakitumiapo Kiswahili. Kama mtafiti wa kazi hii alivyotangulia kusema kuwa kwa ufahamu wake , lugha ya Kinyamwezi haikuwa imefanyiwa utafiti wa kina kuhusiana na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili. Hivyo basi, utafiti huu utatoa mchango mkubwa kwa watafiti wengine kuhusiana na athari za lugha juu ya lugha ya kiswahili.

## 5.4 Mapendekezo:

Baada ya kukamilisha kazi nzima ya utafiti na kupata majibu ya maswali ya utafiti na lengo la utafiti kutimia.Mtafiti anatoa mapendekezo ya jumla kuhusu matokeo ya utafiti na mapendekezo ya tafiti zijazo

### 5.4.1 Mapendekezo ya jumla.

Walimu wafundishao Kiswahili kama lugha au kama somo wajitahidi kupiga msasa lugha yao ili kuhakikisha kuwa wana umilisi wa kutosha wa lugha hiyo,wateue na kutumia ipasavyo mbinu za kufundishia na kuhakikisha wanatayarisha na kutumia vema zana za kufundishia na kujifunzia wakati wa tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji.

Vilevile Jamii,koo,wazazi na wanafunzi, waelimishwe kuhusu faida za lugha ya Kiswahili na matumizi yake kwa mtu binafsi,familia,koo,jamii taifa na kimataifa (uhamasishaji ufanyike kwao ili kuwaibulia ufahamu huo).Waelimishwe juu ya umuhimu wa somo la Kiswahili. Wazazi,jamii,Serikali na wadau wengine wa elimu kwa ujumla waweke utaratibu kuhakikisha kuwa Walimu wafundishao Kiswahili vema zaidi na wanafunzi wafauluo vizuri sana somo la Kiswahili wawe wakipewa motisha zenye tija.

### 5.4.2 Mapendekezo ya tafiti zijazo.

Kama mtafiti wa kazi hii alivyotangulia kusema kuwa kwa ufahamu wake, lugha ya Kinyamwezi haikuwa imefanyiwa utafiti wa kina kuhusiana na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili, utafiti huu ulikusudia kuchunguza Athari za Kinyamwezi Katika Kujifunza Kiswahili. Hata hivyo, utafiti huu haukushughulikia athari zote bali umeshughulikia vipengele vya kiisimu vitatu tu yaani athari za kimsamiati, kimatamshi na kimaana. Hivyo kuna vingine vimebaki vikiwemo vya kisintaksia na kimofolojia vinayohitaji kutafitiwa.

Mapendekezo ya mtafiti ni kwamba vipengele hivyo vilivyoshughulikiwa vinaweza kutafitiwa kwa kutumia nadharia nyingine ili kuchunguza na kuonyesha kwa undani zaidi athari hizo. Aidha, kuna haja ya kufanya tafiti za kina zaidi ili kubainisha athari mbalimbali zikiwemo za kimaumbo na kisarufi kwa ujumla, sababu za athari hizo na mbinu za kuwasaidia Wanyamwezi wanaojifunza lugha ya Kiswahili. Vilevile itakuwa ni vema zaidi kama tafiti mbalimbali juu ya Athari za Lugha Mama mbalimbali za Kibantu Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili zitafanywa ili kusaidia kuondoa dosari katika uzungumzaji wa lugha ya Kiswahili na hivyo wazungumzaji wote wa Kiswahili wawe wakizungumza Kiswahili Sanifu.

### 5.5.Hitimisho.

Kupitia kufanyika kwa utafiti huu,matokeo yaokeo yamedhihirisha Athari za Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Kiswahili,visababishi vya athari hizo mbinu za kutumia ili kuwasaidia wanafunzi wanyamwezi wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili.Makosa yanayofanywa na wanafunzi hao wazungumzapo Kiswahili yafaa yshughulikiwe kwa kuwa kila kosa lina kisababishi chake.

**MAREJELEO**


Babbic, E. (1999), *The Basics of Socil Research*. Belmont Wadsworth Publishing Company

Besha, R.M. (1995), *Uingizaji wa Maneno Mageni Katika Kiswahili*.Kioo cha Lugha, Juzuu 1.Na 1.199

[ *Chombozi.blogspot.com>2013/11 ]* Agosti 30, 2015.

Cohen, L. ( 2000), *Research Methods in Education* (5thed) Londn.. Rontledge press.

Dimmendaal, J. G (2011), *Historical Linguistics and the Comparative Stages.*University of Cologne.

Fletcher, P. and Garman, M. (1986). *Language Acquisition*.Cambridge University Press.

Guthrie, M. (1948), *Classificassion of Bantu Lang*uages. London,Donson of pall mall.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004).*Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.*Nairobi Phoenix Publishers LTD.

Obara, M. J. (2014), *Uchanganuzi wa Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi Wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii.Chuo Kikuu Cha Nairobi [*Erepository.uonbi.ac.ke ] Julai 12,2015.

Kapinga, M. C. (1983), *Sarufi ya Kiswahili Sanifu*.Dar es salaam.

Kihore, Y. M (2003), *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (*SAMAKISA)*.TUKI. Dar es salaam.

Kihore, Y. M. (2001), *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA*).*Sekondari na Vyuo*.Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).Dar es salaam.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A. ( 2006), *Proposal and Thesis Writing : Introduction.* Nairobi, Paulines Publications Africa.

Kothari, R. C. (1990), *Reseach Methodology,Methods and Techniques*. New Delhi. New Age International (P) Limited.

Kothari, R. C. (2008), *Research Methodology; Methods.* New Delhi New Age International Publishing LTD Techniques.

Krashen, S. D. na Tracy D. T. (1983), *The Natural Aproach Language Acquisition in The Classroom.* PergamonPress.Oxford.

Lusesa, J. (2013), A*thari ya Lugha ya Kisukuma Katika Kujifunza Kiswahili*. [www.academia.edu/5555140/Tasnifu_lusesa].Aprili 10,2015

Maganga, C. (1997*), Historia ya Kiswahili*.Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Masebo, J. A. na Nyangwine, N. (2008), *NADHARIA YA LUGHA.KISWAHILI 1.Kidato cha 5 Na 6*.Nyambari Nyangwine Publishers.Dar es salaam.

Massamba, D. P. B. (2002, *Historia ya Kiswahili*. Nairobi Jomo Kenyatta foundation.

Massamba, D. P. B. (2004), *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*,TUKI,Dar es salaam.

Matinde, R. S, (2012), *DAFINA YA LUGHA.ISIMU NADHARIA.Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*.Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Mayala, M. B. { 1971), *Sukuma Expression of Traditional Religion in life*.East Africa.

Mekacha, R. D. H (2000*), Nadharia na Muktadha wa Kiswahili*.Osaka University of Foreign Studies.

Mgullu, R. S. (1999*). MTAALA WA ISIMU:Fonetiki,Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*.Nairobi Longhom Publishers.

Msanjila, Y. P. (2009). *Isimu Jamii.Sekondari na Vyuo*.TUKI.Dar es salaam.

Musau, M., and Leonard, M, C. (2001), *Mbinu za Kisasa za Kufundishia Kiswahili*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es salaam

Nkwera, F. M. V. (1978, *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo*.THP

Tuntufye, N. D. (2010), *Jinsi Ya Kufundisha Kiswahili Darasani.*Tanzania Publishing House; Dar es salaam.

TUKI (1990).*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*.TUKI.Dar es Salaam.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.Toleo la Pili*.Oxford University Press.Nairobi.

William, L. A. (1913), *Athari za Sheng Kwa Lugha ya Kiswahili.* [www.academia.edu/9499200/PENDEKEZO LA UTAFITI].Aprili 10, 2015

Yin, R.K (1994), *Case Study Research Design and Methods (2nd eds);* Thousand Oaks Calif .SAGE Publisher.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATANISHO NA. 01. BAJETI.

| **NAMBA** | **SHUGHULI** | **KIASI CHA FEDHA** |
|---|---|---|
| 1. | Usafiri | 500,000/= |
| 2. | Chakula | 200,000/= |
| 3. | Vifaa na uchapaji | 800,000/= |
| 4. | Gharama zinginezo | 500,000/= |
| JUMLA | | 2,000,000/= |

## KIAMBATANISHO NA.02. RATIBA YA MUDA WA UTAFITI

| KAZI | DES | JAN | FEB | MACH | APR | MEI | JUNI | JUL | AGOST | SEPT | | NOVEMBA | DESEMBA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mada iliyoteuliwa kwa utafiti | | | | | | | | | | | | | |
| Utafiti kuhusu yaliyoandikwa kuhusu mada. | | | | | | | | | | | | | |
| Kuandika Pendekezo la Utafiti | | | | | | | | | | | | | |
| Kukusanya Data. | | | | | | | | | | | | | |
| Kuwasilisha na kuchanganua Data. | | | | | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuwasilisha mswada wa kwanza wa Tasifu. | | | | | | | | | | | | | |
| Marekebisho ya mswada. | | | | | | | | | | | | | |
| Kuwasilisha nakala nne za Tasinifu zilizounganishwa. Utetezi wa Tasnifu | | | | | | | | | | | | | |
| Wasilisho la mwisho la Tasnifu zilizounganishwa | | | | | | | | | | | | | |

## KIAMBATANISHO NA: 03

## MASWALI KWA WANAFUNZI WANYAMWEZI WA SHULE ZA SEKONDARI WANAOJIFUNZA SOMO LA KISWAHILI.

Mimi ni mwanafunzi wa somo la Isimu ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.Ninafanya Utafiti juu ya **Athari za Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili.**Hii ni sehemu ya mahitaji ya kukamilisha masomo yangu ya *Shahada ya Uzamili*.Hivyo ninaomba ushirikiano wako wa kujibu maswali haya ili yasaidie kukamilisha utafiti huu.Toa habari za kweli bila woga wowote.Usiandike jina lako.Habari zozote zitashughulikiwa kama siri na zitatumika kwa utafiti huu tu.Ninatanguliza shukurani za dhati kwa ushirikiano wako.

**Umri.......................................**

**Jinsia......................................**

**Kidato....................................**

**Tafadhali chagua herufi ya jibu kisha uiandike kwenye mabano.Kwenye swali la sita ikiwa jibu lako ni N*diyo* , jaza pia nafasi zilizo wazi.**

1. Je, wewe ni mtu wa kabila la Kinyamwezi?

   (A) Hapana (B) Ndiyo ( )

2. Je, Kinyamwezi ni lugha ya kwanza kwako?

A) Hapana (B) Ndiyo ( )

3. Je, Kiswahili ni lugha ya pili kwako?

A) Hapana. (B) Ndiyo ( )

4. Uwapo nyumbani ni lugha ipi huwa unaitumia zaidi katika mawasiliano?

A) Kiswahili B) Kinyamwezi. ( )

5. Uwapo nyumbani ni lugha ipi huwa unaitumia zaidi katika mawasiliano?

A) Kiswahili B) Kinyamwezi. ( )

6. Unapokuwa nje ya mazingira ya nyumbani na ya shuleni ni lugha ipi uitumiayo zaidi katika mawasiliano?

A) Kiswahili B) Kinyamwezi. ( )

7. Je, ni kweli kuwa Kinyamwezi kimekiathiri Kiswahili kimsamiati?

A) Hapana B) Ndiyo ( )

Iwapo jibu lako ni ndiyo, taja maneno matano ya lugha ya Kinyamwezi yanayotumika katika lugha ya Kinyamwezi .

i. ………………………………………………………………………………

ii. ………………………………………………………………………………

iii. ………………………………………………………………………………

iv. ………………………………………………………………………………

v. ……………………………………………………………………………….
.

## KIAMBATANISHO NA: 04

## MASWALI KWA WALIMU WAFUNDISHAO SOMO LA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI.

Mimi ni mwanafunzi wa somo la Isimu ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.Ninafanya Utafiti juu ya **Athari za Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili.**Hii ni sehemu ya mahitaji ya kukamilisha masomo yangu ya *Shahada ya Uzamili*.Hivyo ninaomba ushirikiano wako wa kujibu maswali haya ili yasaidie kukamilisha utafiti huu.Toa habari za kweli bila woga wowote.Usiandike jina lako.Habari zozote zitashughulikiwa kama siri na zitatumika kwa utafiti huu tu.Ninatanguliza shukurani za dhati kwa ushirikiano wako.

**Umri.................................................................................**

**Jinsia...............................................................................**

**Kiwango cha elimu....................................................................**

**Tafadhali chagua herufi ya jibu kisha uiandike kwenye mabano, jaza pia nafasi zilizo wazi.**

1. Je, kuna athari yoyote ya Kimsamiati, Kimatamshi na Kimaana iliyosababishwa na Kinyamwezi katika kujifunza Kiswahili?.

   a) Hapana (b) Ndiyo ( )

Iwapo jibu lako ni **ndiyo**, toa mifano mitano kwa kila kipengele ili kudhihirisha athari hiyo.

a) Athari ya Kimsamiati:

i. …………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………
………………………………………………………………………..

ii. …………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………
………………………………………………………………………..

iii. …………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………

iv. …………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………

v. …………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………
………………………………………………………………………..

b)Athari ya Kimatamshi:

i. …………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………

ii. …………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………....

iii. …………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

iv ……………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………….

………………….......................................................................................

v …………………………………………………………………………………

... ……………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………

c) Athari ya Kimaana:

i.………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………

ii.………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………....

iii…………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………..

iv , ……………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………….

……………………….......................................................................................

v . ………………………………………………………………………………

... ………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………….

3. Ni sababu zipi huchangia kuwaathiri wanafunzi wanyamwezi katika kujifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili? Taja sababu tano.

i. ………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………..

ii. …………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………..

iii. ………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………….

iv . …………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………….

v . ………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………..

4..Mbinu gani zitumike ili kuwasaidia wanafunzi wanyamwezi wanaojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili? Taja mbinu tano.

i.………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………….

ii………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………..

iii………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………….

iv……………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………………

v………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………….

## KIAMBATANISHO NA: 05

## MASWALI KWA WAMILISI WA LUGHA YA KINYAMWEZI WANAOZUNGUMZA LUGHA YA KISWAHILI

Mimi ni mwanafunzi wa somo la Isimu ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.Ninafanya Utafiti juu ya **Athari za Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili.**Hii ni sehemu ya mahitaji ya kukamilisha masomo yangu ya *Shahada ya Uzamili*.Hivyo ninaomba ushirikiano wako wa kujibu maswali haya ili yasaidie kukamilisha utafiti huu.Toa habari za kweli bila woga wowote.Usiandike jina lako.Habari zozote zitashughulikiwa kama siri na zitatumika kwa utafiti huu tu.Ninatanguliza shukurani za dhati kwa ushirikiano wako.

**Umri……………………………….**

**Jinsia……………………………..**

**Kiwango cha elimu…………………………………………**

**Tafadhali chagua herufi ya jibu kisha uiandike kwenye mabano, jaza pia nafasi zilizo wazi.**

1. Je, wewe ni mzungumzaji mzawa wa lugha ya Kinyamwezi?

(A) Hapana (B) Ndiyo ( )

**Lugha inayotumika zaidi katika mawasiliano na wanafamilia yako uwapo nyumbani ni:**

(A) Kiswahili (B) Kinyamwezi ( )

2. Je, wanafamilia wanyamwezi wanaojifunza Kiswahili huongea Kiswahili sanifu?

   (A) Hapana (B) Ndiyo ( )

Iwapo jibu ni hapana, eleza dosari zinazojitokeza wakati wanapozungumza zinazotokana na ujuzi wa kuzungumza lugha ya Kinyamwezi.

…..........................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

...............................................................................................................

3. Kwa nini wanafunzi wanyamwezi wameathiriwa na Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili? Eleza kwa ufupi ukitumia mifano kisha orodhesha maneno matano (5) yanayoonyesha athari ya lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza Kiswahili:

.............................................................................................................................

.............................................................................................................................

............................................................................................................................